




UKURASA 5

**RC** awachunguza wanyofoaji wa viungo vya maiti mochwari


Nipashe TESA
Jumanne Februari 28, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 12
UNFPA, WiLDAF yawa mkombozi mabinti waliokatishwa masomo
Ukurasa 13
Wadau wanaokereka waja juu, sheria ifute adhabu hiyo inayowaumiza wanafunzi
Ukurasa 14
Waunda shirika, wapiga hodi nyumba kwa nyumba kudai haki, ulinzi wao kisheria
ELIMU
NA WAANDISHI WETU
Ndiyo au hapana kwa viboko shuleni, si uamuzi unaopatikana kwa urahisi

UKURASA 11

# Nipashe


Jumanne Februari 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581235

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Dk. Slaa aibukia CHADEMA bila kadi

**APANDA** jukwaani akiinanga CCM...*Endelea ukurasa 2*



Dk. Willibrod Slaa

ITV Daima

UKURASA WA 3

## ITV, THE GUARDIAN LIMITED ZASHINDA TUZO SUPER BRAND

KAMPUNI za ITV na The Guardian Limited zimetunukiwa tuzo za utendaji bora wa kazi katika tuzo zinazotolewa na Kampuni ya Super Brand...

## Mbaroni kwa tuhuma kuharibu altare, kumwaga sakramenti

UKURASA 5

UKURASA WA 10

## BABA ASHIKILIWA TUHUMA KULAWITI WATOTO WAKE

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia, Haule Abel (38), mkazi wa Ngokolo Manispaa ya Shinyanga kwa tuhuma za kulawiti watoto wake wawili (majina yamehifadhiwa). Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani...



Wananchi wa Kijiji cha Mwaya wilayani Kilombero wakiwa wamekusanyika ofisi za mashamba ya mpira yanayomilikiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kuwalalamikia wafanyakazi wa mashamba hayo wanaodaiwa kumpiga na kumjeruhi mmoja wa wananchi aliyepita kwenye njia zinazopita shambani jana. Mkuu wa Wilaya hiyo, Dunstan Kyobya ameagiza kukamatwa kwa uongozi wa shamba hilo ili umtibu majeruhi na kutofungua njia hizo. **PICHA: IDDA MUSHI**






## UGOMVI VIGOGO WIZARANI

# Rais: Nimechoka kudekeza, safari hii mtaondoka wote

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAPANIA 6 KWA BAMAKO, US MONASTIR UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Rais: Nimechoka kudekeza, safari hii mtaondoka wote

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaapisha viongozi wakuu wa wizara aliowateua juzi, akitaja sababu ya mabadiliko hayo kuwa ni ugomvi kati yao wizarani, akiwaonya ni mara ya mwisho kuwadekeza.

"Ni jambo ambalo silipendi mtu kutokuelewana, mawaziri na manaibu na makatibu wake, sasa ni mwisho kutumia kupangua mmoja mmoja kwenye wizara. Ikitokea tena, mtaondoka wote kwa pamoja!

"Hili silipendi, sasa ninataka nikiwapanga mfanye kazi, sioni sababu ya kutokuelewana, sizielewi sababu zenu za kutokuelewana," alitamka Rais Samia katika lugha ya ukali, akiorodhesha sababu nyingine nne zilizochangia mabadiliko hayo.



Rais Samia alitoa angalizo maalum kwa Wizara ya Uvuvi na Mifugo, akitamka: "(Waziri Abdallah) Ulega nikuombe sasa ule ugomvi wangu nanyi nenda mkafanye kazi!"

Katika orodha ya sababu hizo, Rais Samia kwenye hotuba yake hiyo jana iliyochukua muda mfupi Ikulu, alitaja sababu nyingine ni kumteua Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Madini, baada ya kubaini kuwapo kusuasua kwa uthibitisho wake, kutoka nafasi ya kukaimu, yeye Rais akiwa ameshaagiza muda mrefu.

Vilevile, akataja sababu ya tatu kuteua wasomi na wenye uelevu, ni kwenda kutumia stadi zao serikalini, pia ni fursa ya kujibu kauli kinzani kutoka nje ya serikali, wahusika hao kushuhudia uhalisi na magumu yaliyomo kwenye nafasi hizo.

"Hakuna Mtanzania asiye na akili, kila mtu mwenye akili tutamchukua na kila mmoja ana akili. Wakiwa nje huko wanazungumza, nao sasa tumewaleta ndani waje watupe ubunifu wao na waone ugumu ulivyo," alitamka Rais katika hotuba yake hiyo, iliyobeba utashi wa kupashana ukweli.

Rais Samia alitaja sababu ya nne inahusiana na maboresho katika mfumo wa kiserikali, jukumu la uwekezaji linahamishiwa ofisini kwake kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Alifafanua, katika hatua ya kwanza amemteua Katibu Mkuu kuweka mazingira stahiki kabla ya kumteua waziri mwenye dhamana. Vilevile, vitengo vyake vingine, Tume ya Uwekezaji Tanzania (TIC) na Tume ya Mipango.

"Sekta ya Mifugo na Uvuvi tuone inafanya kazi, kama ulikuwa unafanya ukiwa chini ya mtu, sasa ukafanye na tutaona, nikuombe ukafanye hiyo kazi.

"Niwapongeze manaibu waziri, sio kwamba hamna kosa ila mama analea. Mabadiliko ni kawaida ili kuimarisha serikali na kufikia kasi inayotarajiwa," alisema.

Katika orodha ya walioteuliwa ni: Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ambaye anakuwa waziri, Hamis Mwinjuma, maarufu Mwana FA, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, akichukua nafasi ya Pauline Gekul aliyehamishiwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Baada ya kiapo hicho viongozi hao walikula kiapo cha uadilifu. Rais Samia alifanya mabadiliko madogo kwenye Baraza lake la Mawaziri, makatibu wakuu na wakuu wa mikoa na taasisi za serikali juzi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 02-03-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 203 DYJ / T 394 DVS / T 460 DYG / T 879 EAU T 681 DUB / T 881 EAU / T 792 DYL / T 321 DDH / T 660 BZU / T 236 BYM**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 23.00** |
| **Upana** | - | **mita 5.10** |
| **Kimo** | - | **mita 5.60** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 02-03-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga kupitia Mlandizi** gari hiyo ina namba ya usajili: **NRB 97300 / NRB 54202**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 22.30** |
| **Upana** | - | **mita 5.35** |
| **Kimo** | - | **mita 4.70** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga kupitia Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*


# Dk. Slaa aibuka CHADEMA bila kadi

**Na Waandishi Wetu,** KARATU

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Balozi Dk. Wilbroad Slaa, amerejea kimyakimya kwenye siasa za upinzani baada ya miaka minane, akitaka chama hicho kisibezwe kwa kuwa serikali inatumia baadhi ya sera za chama hicho.

Katika hali ambayo haikutegemewa na wengi kutokana na misimamo yake wakati anajiondoa CHADEMA miaka minane iliyopita, jana Dk. Slaa ambaye alikuwa Balozi wa Sweden tangu Novemba 23, 2017, aliibuka katika mkutano wa chama hicho uliofanyika Kata ya Rhotia wilayani Karatu mkoani Arusha.

Dk. Slaa aliondoka CHADEMA mwaka 2015 baada ya chama hicho kumpitisha Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa kuwa mgombea wa nafasi ya urais, akidai uamuzi huo ulikuwa kama usaliti kwa chama hicho.

Dk. Slaa hakuishia hapo, hivi karibuni alichapisha kitabu kinachoelezea maisha yake, kikiwa na kichwa 'Nyuma ya Pazia - CHADEMA ilivyosalitiwa 2015', akifafanua mambo mbalimbali yaliyojiri wakati wa uteuzi wa Lowassa miaka minane iliyopita.

Jana Dk. Slaa aliwahutubia wananchi huku akijitambulisha kuwa yeye ni profesa wa siasa za Tanzania.

"Atakayehitaji huduma yangu kwa sasa nitampa kwa sababu mimi kwa sasa ni profesa wa siasa, kazi yangu ni kutoa ushauri, nitawaelekeza kwa kuwa profesa aliwahi kupitia mengi, magumu ana uzoefu wa namna ya kutatua, ndio maana wazee vijijini wamekula chumvi, mtu na mkewe wana ugomvi wanakimbilia kwa mzee.

"Sasa kama waliona kuna umuhimu niongee nilikubali, ninajua haki zangu, hakuna wa kuniuliza kwanini umeongea na CHADEMA. Ninaongea pale nina imani moyoni mwangu kuwa ninawatendea haki Watanzania, nitasema bila kumung'unya maneno.

"Nendeni dukani, bei ya mchele ni Sh. 3,500, mlishawahi kuona bei ya namna hiyo? Mchele unalimwa Mang'ola halafu unanunua bei hiyo. Kuna wengine wameacha kula wali. Bei ya nyama Sh. 9,000, mna mgodi wa hela?" Dk. Slaa aliwauliza wananchi waliokuwa wanamsikiliza.Katika mkutano huo, Dk. Slaa alihoji kama sera ya CHADEMA inakubalika, akitamka: "Nani atasema hakijakomaa, wakati ni chama kikuu cha upinzani?"

Alisema kama sera ya chama hicho inapokewa na kugeuka kuwa Sera ya Taifa, CHADEMA kisibezwe kwa kuwa serikali inatumia sera nyingine kutoka chama hicho na anayesema chama hicho hakijakomaa kushika nchi, hayuko sawa.

"Hayati Rais Benjamin Mkapa alikuwa anazindua Hospitali ya Wilaya, baada ya kumsomea tafsiri ya sera za CHADEMA, alisema mbunge (Dk. Slaa) ninaomba kitabu cha sera zenu (CHADEMA), tukaenda kwenye majumuisho ya ziara ya Rais Arusha, alitangaza sera ya afya kwa kutumia sera ya CHADEMA.

"Kwa muundo huu, nani atasema CHADEMA haijakomaa kushika nchi? Kama sera ya CHADEMA inapokewa, inageuka kuwa sera ya Taifa, ni kwanini wasifikie hatua ya kutangazwa hiki ni chama kikuu na kina uwezo wa kuongoza taifa? Matokeo yake tunaona wananyimwa hata haki ya kufanya mikutano," alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu kutoa ufafanuzi kuhusu mkutano alioshiriki Dk. Slaa, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alikiri mwanasiasa huyo kupewa fursa ya kuzungumza katika mkutano huo.

Golugwa alisema sababu iliyomsukuma Dk. Slaa kupanda jukwaani ni mradi wa maji aliouanzisha ambao umekuwa na matatizo mengi ya uendeshaji.

"Serikali imeuchukua mradi huo baada ya kuwa na malalamiko mengi. Sasa kama mwanzilishi, wazee walimwita kuja kufanya kikao," alifafanua Golugwa.

Alisema Katibu Mkuu huyo wa zamani akiwa njiani ndio alikuta mkutano, naye akajumuika kwenye mkutano huo.

Golugwa alisema suala la uanachama wake hawezi kulizungumza kwa kuwa wanachama wa CHADEMA ni lazima wawe kwenye kanzidata.

"Wale waliokuwa na kadi za zamani wanatakiwa wahuishe kadi zao na yeye (Dk. Slaa) akiwamo," alisema.

Dk. Slaa alikuwa Mbunge wa Karatu kwa vipindi viwili kuanzia mwaka 1995 hadi 2005 na tangu alipotangaza kujiondoa, alikuwa hajapanda kwenye jukwaa la CHADEMA hadi jana alipowahutubia wananchi hao.

***Imeandikwa na Jaliwason Jasson (KARATU) na Godfrey Mushi (ARUSHA)**

## HABARI KITAIFA

# ITV, The Guardian Limited zashinda tuzo Super Brand

**Na Shufaa Lyimo**

KAMPUNI za ITV na The Guardian Limited zimetunukiwa tuzo za utendaji bora wa kazi katika tuzo zinazotolewa na Kampuni ya Super Brand.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wa kutoa tuzo hizo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Super Brand Afrika Mashariki, Jawad Jaffer, alisema ametoa tuzo hizo kutokana na kuridhishwa na utendaji kazi wa kampuni hizo kwa mwaka jana.

"Tumetoa tuzo hizi kutokana na utafiti tulioufanya na kuridhishwa na utendaji kazi wa kampuni ambazo tumeona zinastahili ushindi wa tuzo hizi," alisema.

Mkurugenzi huyo alizitaka kampuni nyingine ambazo hazijafanikiwa kupata tuzo hizo, ziongeze juhudi ili zipate nafasi kama hiyo mwakani.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo, Mwakilishi wa Kampuni ya The Guardian Limited, Alex Songa, alisema amefurahi kwa kampuni kupata tuzo hiyo ambayo itaongeza juhudi ya kufanya vizuri zaidi.

"Tuzo hii nzuri kwetu na itatufanya tuzidi kupambana zaidi, tunaahidi hatutawaangusha, tutakuwa bora zaidi," alisema Songa.

Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul, alishukuru kupata tuzo hiyo na kuahidi kuboresha zaidi vipindi vyao viendelee kukidhi matarajio na matakwa ya watazamaji na wasikilizaji.

"Hii ni mara yetu ya sita kupata tuzo hii, tunaishukuru Kampuni ya Super Brand Afrika Mashariki kwa kutuamini na kutupa tuzo ambayo itatufanya tuzidi kupata hamasa ya kuboresha vipindi vyetu," alisema Paul.

Mwakilishi wa Kampuni ya ASAS, Jimy Kiwelu, alisema tuzo hiyo itawafanya wazidi kutengeneza bidhaa bora zaidi, ili kupeperusha vyema bendera ya Tanzania kitaifa na kimataifa.

Kampuni nyingine zilizotunukiwa tuzo hizo ni Red Gold, Petro Group, White dent na Azam TV.




Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul (kushoto) na mwakilishi wa The Guardian Limited, Alex Songa wakiwa na tuzo za Super Brand baada ya kampuni hizo mbili kuibuka washindi kufuatia utafiti uliofanywa na Super Brand Afrika Mashariki mwaka 2022 katika hafla ya utoaji zawadi iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

HBS Hannah Bennie Schools

# OPEN JOB VACANCIES - WE ARE HIRING

- ✓ SCHOOL BUS DRIVER (4)
- ✓ CHEF (2)
- ✓ EXTRA CURRICULAR COORDINATOR (2)
- ✓ ICT TEACHER/ADMINISTRATOR (2)
- ✓ ADMIN & CUSTOMER SERVICES OFFICER (2)

* School bus driver must have vehicle technical skills (fundi)
* Extra-curricular coordinator oversees /coach sports, music, performing art, etc.
* ICT teacher/ admin candidate must have excellent systems/ network admin skills and teaching passion.
* Admin/customer service officer must have excellent / aboveaverage computer/ MS office skills and passion for customer services.




**PHONE CALLS related to Job advert are NOT ALLOWED !** Please send all your enquiries to the email address **hr.hbs.tz@gmail.com**

# TCDC yaja na mkakati wa kukuza biashara kidijitali

Na Mwandishi Wetu

KAMISHENI ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) imeanza kutekeleza mpango wa kubadili namna ya kuendesha vyama vya ushirika na kuviwezesha kutumia teknolojia za kisasa katika kufanya shughuli zao.

Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo, Abdulmajid Nsekela, alitoa taarifa hiyo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa ushirika kujadili maendeleo ya ushirika na kuweka mkakati wa kuimarisha sekta ya hiyo nchini.

Nsekela alisema uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali utaongeza ufanisi wa kiutendaji katika Vyama vya Ushirika pamoja na mamlaka za usimamizi wa sekta hiyo.

Aliongeza kuwa pamoja na mambo mengine, mapendekezo yatakayotolewa katika mkutano huo yatasaidia kuuboresha mfumo wa Ushirika kuwa wa kisasa zaidi ili kuwawezesha wananchi kushiriki ipasavyo kwa ustawi wao na wa taifa kwa ujumla.

"Ni matumaini yangu kuwa maazimio yatakayofikiwa kupitia mkutano huu yatapaswa kutekelezwa ipasavyo na kila mdau na taarifa ya utekelezaji itakuwa inatolewa na kujadiliwa mara kwa mara," alisema Nsekela.

Mrajisi wa Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alisema lengo kubwa la mkutano huo wa wadau wa Ushirika ni kujadili maendeleo ya Ushirika na kuweka mkakati wa kuimarisha sekta hiyo nchini.

"Mkutano huu ni muhimu kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo ya ushirika nchini, lakini tumekutana wadau wote ili kuja na mapendekezo ya pamoja ya kuendeleza sekta hii kwa maendeleo ya taifa," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifafanuliwa jambo na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa kiwanda cha kuchakata mafuta ya mawese cha Trolle Messle, Daniel Amulike, alipotembelea kiwanda hicho kuona mtambo wa kukaushia mbegu za zao la chikichi mjini Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madalali wadaiwa kuwadhalilisha kingono wafanyakazi wa ndani

Na Christina Mwakangale

MABINTI wanaofanya kazi za ndani wameiomba serikali ipige marufuku madalali wanaotumika kuwezesha kupatikana kwao, wakidai wanashusha utu wa mwanamke.

Wamesema baadhi yao huwarubuni kwa rushwa ya ngono kwa ahadi ya kuwatafutia kazi nzuri, mshahara mnono na katika miji mikubwa, likiwamo Jiji la Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Shirika la Light for Domestic Workers, Beatrice Johnson aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kongamano la kuadhimisha miaka 15 ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T).

Alisema shirika hilo linalofanya shughuli zake mkoani Morogoro, limeshawafikia waajiri 72 na wafanyakazi wa ndani 250 kuwapa elimu kuepukana na ukatili wa kijinsia kama vile rushwa ya ngono na mimba.

"Hawa madalali wanaotumika kuwatafutia kazi mabinti, wamekuwa wakiwarubuni wasichana, utakuta wanakwenda maeneo tofauti mikoani kuwachukua wasichana na kuahidi kazi nzuri.

"Kutokana na wazazi kuahidiwa hayo, anamtoa mwanawe ili aje mjini kutafuta fedha kwa kufanya kazi za ndani. Madalali hawa walio wengi wanatambulika na mtu unawaamini, ila baadhi yao wanawaambia ukitembea naye anakupa kazi," alisema Beatrice.

Alisisitiza kuwa jamii inapaswa kufahamu kwamba Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004 inamlinda mfanyakazi wa nyumbani akiwamo mwenye umri wa miaka 14, ingawa changamoto ni wenye umri huo kufanya kazi zisizoendana na umri wao.

# Majeruhi ajali ya mwendokasi atoka Muhimbili

Na Christina Mwakangale

MMOJA wa majeruhi walio lazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutokana na ajali iliyohusisha magari mawili, likiwamo la mwendokasi, ameruhusiwa kutoka huku wawili wakiendelea na matibabu hospitalini huko.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano MNH, Neema Mwangomo, aliiambia Nipashe jana kwamba mmoja wa majeruhi ameruhusiwa na wawili wanaendelea vizuri na afya zao zinaimarika.

Taarifa iliyotolewa na MNH baada ya ajali hiyo, ilibainisha kuwa hospitali hiyo ilipokea majeruhi 37. Kati yao, 24 ni wanafunzi na watu wazima 13 huku 27 wakiruhusiwa kurejea nyumbani, saba wakipewa rufani kwenda Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI).

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, alibainisha juzi kwamba hadi Jumamosi, ndugu wa majeruhi wa ajali hiyo aliyelazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) cha taasisi hiyo, walikuwa hawajajitokeza.

"Majeruhi huyu bado yupo ICU na afya yake inaendelea kuimarika lakini ndugu zake mpaka sasa hawajajitokeza," alisema.

Ajali hiyo ilitokea Jumatano ya wiki iliyopita, eneo la Kisutu jijini Dar es Slaam, ikihusisha gari ndogo aina ya Rav 4 lenye namba ya usajili T 978 DHZ na basi la mwendokasi lenye namba za usajili T 122 DGW.

Video fupi iliyorekodi tukio hilo lililotokea majira ya saa 12:31 asubuhi, ilionyesha namna ajali hiyo ilivyotokea kwa magari hayo kugongana, basi la mwendokasi likipoteza mwelekeo. Basi hilo lilikuwa linatoka Kivukoni kwenda Kimara.

**Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, alibainisha juzi kwamba hadi Jumamosi, ndugu wa majeruhi wa ajali hiyo aliyelazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) cha taasisi hiyo, walikuwa hawajajitokeza.**

# Timu uchunguzi unyofoaji viungo vya maiti yaundwa

**Na Waandishi Wetu,** MANYONI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amefikishiwa kilio na wananchi wa Wilaya ya Manyoni mkoani Singida cha mauaji ya kikatili huku serikali ikibainisha hatua zilizochukuliwa ikiwamo kuunda timu ya kuchunguza matukio hayo na ya unyofoaji wa baadhi ya viungo vya maiti.

Kilio hicho kiliibuliwa jana na mmoja wa wananchi kwenye mkutano wa kusikiliza kero za wananchi, Chongolo alipotembelea shina namba tano la Kata ya Manyoni.

Akizungumzia suala hilo, Chongolo alisema CCM imepewa dhamana ya kuwalinda wananchi na jambo hilo limeainishwa kwenye ilani yake yenye kurasa 303 na kutaka Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba kutoa majibu ya malalamiko hayo.

Serukamba alisema mauaji mengi yanayotokea kwenye eneo hilo yanahusisha imani za kishirikina na yanahitaji uchunguzi wa kisayansi ili kuyatatua.

"Niliunda timu inayoshirikisha watu mbalimbali ambayo inajumuisha vijana wa nje kabisa ya eneo hili, tunafuatilia ili kujua chanzo cha mauaji haya na kila atakayebainika kuhusika kwenye mauaji haya hatutakuwa na msalia mtume kwenye hili ili kuhakikisha usalama wa eneo hili unaimarika," alisema.

Serukamba alisema kuwa mbali na mauaji hayo, pia kuna tabia imeibuka ya watu kuingia chumba cha kuhifadhi maiti na kunyofoa baadhi ya viungo vya mwili kwenye maiti na kusisitiza kuwa serikali itakomesha mtandao wa vitendo hivyo vya uhalifu.

"Niwahakikishie tupo kazini, tunafanyia uchunguzi masuala haya na tutayakomesha, kila ambaye atashukiwa anashiriki katika mauaji haya, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Atakayeshukiwa anatenda mambo haya hatutakuwa msalia mtume, tusianze kupiga kelele wamemkamata babu yangu, hakuna cha mchungaji wala shekhe, kama tukimkamata anahusika tutampeleka vyombo vya sheria," alisema.

Januari 20, mwaka huu, Serukamba alipofanya ziara kusikiliza kero za wananchi, walimweleza kuwa kuna pikipiki zinazodaiwa kutumika katika mauaji hayo.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hapa Manyoni vifo vimekithiri sana, kila wiki lazima tuokote maiti mahala fulani, lakini sio kwamba wananchi wa Manyoni hawawafahamu wahalifu, bali wanawafahamu," alisema Prisca Maleta, mmoja wa wananchi hao.

Katika hatua nyingine, Chongolo alikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Itigi hadi Makongolosi, akiagiza thamani ya fedha ya miradi izingatiwe ili barabara ziwe imara na kujiepusha na marekebisho ya mara kwa mara yanayosababisha gharama kubwa kutumika.

Pia alikemea tabia ya makandarasi kuweka matuta ovyo barabarani hadi kwenye maeneo ambayo hayastahili kuwekwa kwa kuwa si makazi ya watu.

"Tutengeneze namna ya kudhibiti wasiofuata taratibu barabarani badala ya kuweka matuta ambayo sasa yamekuwa ni kero na kuharibu barabara," aliagiza.

***Imeandaliwa na Augusta Njoji na Thobias Mwanakatwe**

# Mbaroni kwa tuhuma kuharibu altare, kumwaga sakramenti

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kuvunja na kuharibu mali za Kanisa Kuu Jimbo Katoliki la Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Geita, Safia Jongo, alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa 8 usiku wa kuamkia Februari 26, mwaka huu.

Alisema mmoja ana umri wa miaka 25 ambaye jina lake limehifadhiwa kwa ajili ya upelelezi, ambaye ni muumini wa kanisa hilo, mlinzi na aliyewahi kuhudumu.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, mtu huyo alikuwa amelewa, alifika kanisani huko usiku wa manane na kuupiga ngumi mlango wa kuingilia ndani ya kanisa hilo.

Alisema mtu huyo alijeruhiwa kwa kioo kwenye mkono wa kulia pamoja na sikio la kushoto.

Kamanda Jongo alisema mtu huyo baada ya kuvunja mlango wa kanisa hilo na kuingia ndani, alikwenda moja kwa moja madhabahuni na kuharibu vitabu vya kanisa na vitambaa wanavyotumiwa na maaskofu.

Alisema mtu huyo aliingia kwenye chumba kinachotunza maji ya baraka akamwaga na kuvunjavunja vitu vyote vilivyokuwamo ndani ya chumba hicho, akaingia chooni na kuharibu kila kitu, juu kulikuwa na kamera za siri (CCTV Camera) akavunjavunja zote pamoja na kuharibu mali mbalimbali za kanisa hilo.

"Ni kweli mtu huyo mwenye umri wa miaka 25 alikuwa katika hali ya ulevi na watu wengine aliokuwa akinywa nao walithibitisha kwamba ni kweli alikuwa amelewa, sawa ni pombe lakini tunaendelea kumshikilia tujue ni kwa nini?" Alisema.

"Vitu alivyovifanya ni vikubwa sana, hata msalaba wa chuma aliweza kuuvunja, nguvu alizokuwa nazo ni kubwa inawezekana alikuwa na kitu ambacho sio cha kawaida ndani ya nafsi yake kama mwenyewe anadai kuwa ni muumini wa kanisa hilo," alisema.

Pia alisema kuwa mtu huyo alikuwa mhudumu wa kanisa hilo na ndio maana anafahamu maeneo mengi ya kanisa hilo na kwamba katika uchunguzi watataka kujua kwanini aliamua kufanya uharibifu huo.

"Tumemwacha pombe ziishe ndipo tuendelee na mahojiano ili kubaini chanzo cha yeye kufanya hivi," alisema.

Kamanda Jongo pia alikemea tabia ya visasi vya kifamilia na kijamii, akisisitiza si jambo zuri.

**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

## TAARIFA KWA UMMA

## Kuondolewa kwa Ukomo wa Matumizi ya Vitambulisho vya Taifa

***Dar es Salaam; Februari 28, 2023***

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapenda kuwafahamisha wananchi wote wenye Vitambulisho vya Taifa ambavyo vina tarehe ya ukomo wa matumizi kwa mujibu wa Kanuni ya 7 (2) (v) ya Kanuni za Usajili na Utamvuzi wa Watu za Mwaka 2014 kwamba, Serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, imeondoa ukomo wa matumizi ya Vitambulisho kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na. 96 la tarehe 17 Februari, 2023.

Hivyo basi, watoa huduma wote nchini wanaotumia Vtambulisho wa Taifa katika kuwahudumia wananchi wazingatie maelekezo ya Serikali ya kuendelea kuvitambua na kuvitumia Vitambulisho vya Taifa ambavyo vina tarehe ya muda wa ukomo uliopita kwa kuwa Vitambulisho hivyo havitakuwa na ukomo wa matumizi.

Marekebisho haya hayahusishi Vitambulisho vya Wageni Wakaazi na Wakimbizi na hivyo muda wa Vitambulisho hivyo uzingatiwe pale vinapotakiwa kuhuishwa.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Mawasiliano na Hifadhi Hati,**
**Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wateule wa Rais watambue dhamana nafasi walizopewa

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alifanya mabadiliko ya uongozi katika nafasi mbalimbali kwa kuwateua watu na hatimaye kuwaapisha jana katika hafla iliyofanyika Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma. Katika mabadiliko hayo wako waliopandishwa kuwa waziri na makatibu wakuu.

Sambamba na hao, wako pia walioteuliwa kuwa makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu wa wizara. Pia wako manaibu mawaziri na makatibu wakuu waliohamishwa kutoka wizara moja kwenda nyingine. Wako pia walioteuliwa kuwa wakuu wa mikoa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na waliokuwamo kutenguliwa au kushika nyadhifa zingine.

Mabadiliko hayo ni sehemu ya mwendelezo anaoufanya Rais mara kwa mara kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha utendaji serikalini. Kabla ya uteuzi wa juzi, hivi karibuni Rais Samia alifanya mabadiliko madogo katika Wizara za Maliasili na Utalii na Utamaduni, Sanaa na Michezo lengo likiwa lile lile ka kuisika serikali ili kuwaletea wananchi maendeleo yaliyokusudiwa.

Mwelekeo wa mabadiliko hayo yanaakisi pia rai aliyoitoa katika Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Desemba, mwaka jana, jijini Dodoma kwamba anakusudia kuisuka serikali yake katika ngazi mbalimbali ili kuboresha utendaji.

Ni dhahiri kwamba mabadiliko hayo aliyoyafanya Rais na yale aliyoyafanya awali, yana nia thabiti ya kuleta maendeleo kupitia sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii na kwamba walioteuliwa kushika nafasi hizo, zikiwamo za watendaji wakuu wa wizara. Kwa mantiki hiyo, wateule hao wameaminiwa kuwa wana uwezo wa kufanya kazi hiyo ndiyo maana kuna wengine walikuwa wakuu wa taasisi nyeti ndani ya serikali na wamepandishwa kuwa makatibu wakuu au naibu makatibu wakuu.

Jambo la msingi wanalopaswa kutambua ni kwamba hadi kufikia hatua ya kuteuliwa, wamepitia katika chujio zito na kuonekana kwamba wanafaa, hivyo waonyeshe kwamba Rais hakukosea kuwapa nafasi hizo. Wanachotakiwa ni kuwajibika ipasavyo kwa kuleta matokeo yanayotarajiwa kupitia nafasi zao na sekta walizopewa kuziongoza.

Aidha, kuna msemo kwamba uongozi ni kuongozwa na watu, hivyo viongozi hao wanapaswa kujua kwamba wao si watawala bali ni viongozi na wanatakiwa kusikiliza matatizo na kero za wananchi kupitia sekta walizopewa kuziongoza. Kwa maneno mengine, wanatakiwa kusikiliza kero zinazowakabili wananchi na kutoa majibu sahihi na kumaliza kero hizo.


Kadhalika, wateule hao wanatakiwa kutambua kwamba nafasi walizopewa ni dhamana kwa kuhakikisha wanazitumia ipasavyo kwa manufaa ya nchi na si kwa maslahi yao. Kwa kutambua hilo, pia wajue kwamba kuna siku watatakiwa kutoa hesabu ya kazi walizofanya na wasipofanya hivyo watatenguliwa au kuondolewa kwenye nafasi hizo kama ilivyofanyika kwa baadhi ya waliotangulia.

Kwa kutambua kwamba wamebeba dhamana nzito ya kuwaongoza wananchi, mawaziri, manaibu mawaziri, makatibu wakuu na manaibu makatibu wakuu hao, wanapaswa kuelewa kuwa kuteuliwa kwao ni heshima kubwa, hivyo watekeleze majukumu yao kwa uwezo wao na kwa weledi wa hali ya juu. Pia wasiweke katika fikra zao kwamba kwa kupewa nafasi hizo 'wameukata' au 'wameula' kwamba wameuaga umaskini au watapata manufaa fulani.

Aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, alipoteua baraza lake la kwanza la mawaziri mwaka 2015, aliwaonya wale wanaofanya sherehe kwa kuteuliwa kuwa mawaziri au naibu mawaziri kwa kudhania kwamba wamepata manufaa na kuwataka pia watakapofukuzwa wafanye sherehe. Kauli hiyo ilidhihirisha kwamba nafasi hizo ni kaa la moto na si za kuzifurahia.

Jambo la muhimu kwa wateule ni kuweka akilini kwamba nafasi walizopewa ni kubwa, nyeti na si lelemama hivyo waombe hekima ili kutekeleza majukumu yao. Wajione kwamba ni watumishi wa wananchi na si mabwana. Kwa kufanya hivyo, watatimiza wajibu wao kwa viwango vya juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vishikwambi vilete tija kwenye elimu

Na Sabato Kasika

**TEKNOLOJIA** ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zama hizi ni kila kitu. Mchango wake ni mkubwa ikiwa ni pamoja kuharakisha kufikia mafanikio kuanzia kilimo, elimu, uchumi na hata mawasiliano.

Duniani sasa kutumia TEHAMA kunalenga kuwa ifikapo 2025 elimu iwe imefika kwa wote, kuwapo na uhakika wa chakula salama, kuwapo kwa mazingira ya amani ili kuwapo kwa jamii bora yenye kujali maisha ya wananchi.

TEHAMA inatumika kila mahali na katika kutoa huduma za aina zote ile ikiwamo kukusanya mapato na taarifa muhimu, elimu, matibabu, biashara, usafirishaji, utafiti na ununuzi wa nishati. Baada ya kuingia kwa utandawazi, dunia sasa ni kijiji kimoja tena kidogo, kwani mawasiliano yameendelea kuboreshwa siku hadi siku, kitendo ambacho kinarahisisha karibu kila kitu.

Ukweli ni kwamba, dunia inahama kwa kasi katika matumizi ya teknolojia, ambapo kwenye eneo la elimu, ni muhimu kuendana na teknolojia ili kupata uwiano bora wa kuboresha huduma ya elimu.

Tanzania haikuwa nyuma inachukua hatua mbalimbali za kuimarisha TEHAMA katika elimu, ikiwamo kugawa vishikwambi 293,400 kwa walimu msingi na sekondari.

Vishikwambi hivyo vimegawiwa kwa walimu hao, kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa njia ya TEHAMA ikiwa ni sehemu ya kuakisi mpango mkakati wa maendeleo wa taifa ambao unaainisha afua ya kimkakati kuboresha na kuimarisha utoaji wa elimu.

Mojawapo ya maeneo ya kipaumbele katika mpango huo, unaelezwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwa ni kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kuboresha maisha ya walimu.

Wakati serikali ikiwa na matarajio hayo, ni vyema wale waliokabidhiwa vishikwambi hivyo kuvitumia kwa kile kilichokusudiwa na pia kuvitunza ili viweze kuleta matokeo chanya katika ufundishaji.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, serikali imewekeza zaidi katika eneo la TEHAMA na kwamba uwekezaji huo umeelekezwa katika maeneo ya miundombinu, vitendea kazi, mitaala na mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji, hasa walimu, ili kuboresha ufundishaji, usimamizi na ufuatiliaji.

Kama anavyoeleza Waziri Mkuu kwamba, kumekuwapo na uhitaji wa vifaa vya TEHAMA, katika shule hasa kwa walimu katika maandalizi ya ufundishaji, usimamizi na upimaji wa sekta ya elimu, suala la kuvitunza vishikwambi hivyo ninaona ni la muhimu.

Wadau wengine wanaotajwa kupata vishikwambi hivyo ni wadhibiti ubora wa shule wilaya na kanda, wakufunzi wa vyuo vya ualimu vya umma na wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC).

Wadau wengine walionufaika na mgawo ni maofisa elimu ngazi ya mkoa, wilaya na kata, wakufunzi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi-VETA na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Pamoja na ushauri wa kuvitunza na kuvitumia inavyotakiwa, ninadhania pia kuna haja serikali kufuatilia kwa karibu maelekezo yake kwamba vinatakiwa kugawiwa kwa walengwa tu na si vinginevyo.

Ninashauri hivyo, kwa sababu kumekuwapo malalamiko ya kutotekelezwa kikamilifu maelekezo ya Waziri Mkuu, kuhusu ugawaji wa vishikwambi hivyo, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema anadai kuyapokea.

Katika ufafanuzi wake anasema, wakati akizindua ugawaji wa vishikwambi hivyo Novemba mwaka jana, Waziri Mkuu aliagiza vifaa hivyo vinakwenda kwa walengwa.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo chama kimepokea malalamiko ya kutotekelezwa kikamilifu kwa maelekezo ya Waziri Mkuu na kuagiza Wizara ya Elimu kuhakikisha vinawafikia walengwa, si vinginevyo.

Haipendezi kuona mwendelezo wa jitihada za serikali kuwawezesha na kuwajengea uwezo walimu kuwa na vitendea kazi na kuimarisha matumizi ya TEHAMA, unachezewa.

Juhudi za kuendelea kuwawezesha walimu kuwa na vitendea kazi na kuimarisha matumizi ya TEHAMA ni za kuungwa mkono, hasa baada ya kuchukua vishkwambi vilivyotumika wakati wa sensa mwaka jana na kuwapa wadau hao wa elimu ili wapige hatua katika ufundishaji na ujifunzaji.

# LATRA yatangaza njia mpya kuboresha usafiri

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza njia mpya za daladala mkoani Dar es Salaam, ikilenga kufikisha huduma hiyo kwenye maeneo ya pembezoni kwenye makazi mpya yanayoendelea kukua.

Taarifa ya LATRA iliyotolewa hivi karibuni imetaja njia ndefu ya daladala inayoanzia Kibada wilayani Kigamboni hadi Tegeta Nyuki wilayani Kinondoni.

Taarifa ya LATRA kwenye tovuti yake imewataka wasafirishaji kuomba leseni kwenye njia hizo mpya.

Taarifa ya LATRA imetaja njia hizo mpya kuwa ni kutoka Kibada stendi Kigamboni kuelekea Mbezi Luis, Simu 2000, Temeke Mwisho, Tabata Segerea, Tegeta Nyuki na Kigogo Sokoni.

Ilieleza kuwa mabasi yatakayoomba njia hiyo, yataanzia safari zake na kushia Kibada stendi kupitia kivuko cha Daraja la Nyerere.

Ilisema magari yatakayofanya safari za Mbezi Luis na Simu 2000 yatapita Daraja la Nyerere hadi barabara za Mandela na Morogoro wakati yatakayoelekea Tegeta Nyuki yatapita darajani, Mandela, Sam Nujoma hadi Bagamoyo.

Njia ya Temeke kwa mujibu wa LATRA, magari yatapita Daraja la Nyerere hadi Barabara ya Kilwa na yale yanayoelekea Kigogo Sokoni, yatapita Mandela kisha Nyerere.

Nyingine kwa mujibu wa LATRA ni kutoka Pugu Stesheni hadi Kawe kupitia barabara za Nyerere, Uhuru na Kawawa.

LATRA pia imetangaza njia kutoka Bunju Sokoni hadi Kawe Ukwamani, Tegeta Nyuki-Kawe Ukwamani, Kigogo Sokoni- Temeke, Kwa Lugwadu – Mbagala Rangi 3 na kutoka Hospitali ya Vijibweni kwenda Muhimbili, Machinga Complex, Mnazi Mmoja, Makumbusho, Simu 2000, Kawe Ukwamani na Tabata Segerea.

"Mamlaka inawataarifu wasafirshaji kuwa imetengeneza na kuidhinisha njia mpya za mabasi ya mjini kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Njia hizi zinategemea kuongeza wigo wa uwekezaji katika usafirishaji wa umma na utoaji huduma kwa wananchi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel (wa tatu kulia), akikata keki kwenye maadhimisho ya miaka 25 ya kituo cha huduma za utengamao kwa watu wenye ulemavu cha CCBRT Moshi mkoani Kilimanjaro jana. Anayeshuhudia, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (wa pili kulia), Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Makori Kisare (kulia) na Rais wa Bodi ya Wakurugenzi wa CCBRT, Dk. Willibrod Slaa (wa nne kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mganga wa kienyeji mbaroni madai kumnajisi mteja wake

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara linamshikilia mganga wa kienyeji, Issa Mando (41), mkazi wa Kijiji cha Chipuputa mkoani hapo kwa madai ya kumnajisi binti mwenye umri wa miaka 17 (jina linahifadhiwa), akimlaghai kumpa tiba.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Hamisi Ramadhamani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana.

Alisema mganga huyo anadaiwa kumlaghai binti hiyo kwamba akimfanyia kitendo hicho, ataondokana na vikwanzo mbalimbali vinavyomsumbua maishani.

Kaimu kamanda huyo alisema binti huyo alikwenda kwa mganga huyo na kumwomba tiba kwa ajili ya kutaka amwondolee matatizo mbalimbali ambayo yanamkabili katika maisha yake.

Alidai mganga huyo alikwenda na binti huyo kwenye moja ya makaburi kijijini huko kwa madai ya kwenda kumpa dawa huku akimwaminisha kuwa tiba atakayompa itamsaidia.

Alisema kuwa walipofika eneo la makaburi, mganga huyo alimlazimisha binti huyo amwingilie kimwili huku akimweleza kuwa ni tiba ambayo alikuwa anahitaji kutoka kwake na ingemsaidia kuondoa matatizo yake.

Kwa mujibu wa Kamanda Ramadhani, polisi baada ya kupata taarifa walimkamata mganga huyo na baada ya upelelezi kukamilika, atafikishwa mahakamani.

Alitoa wito kwa jamii kuacha tabia za vitendo vya ubakaji na kwamba wote wanaojihusisha na vitendo hivyo na kubainika watafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kaimu Kamanda huyo alisema jamii pia inapaswa kutoa ushirikiano kwa polisi kuhusu vitendo vya uhalifu, ili wahusika wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa kuwa kufanya hivyo, vitendo hivyo vitapungua na jamii itaishi kwa amani na upendo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# China yaahidi kupokea maharage na parachichi kutoka Tanzania

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya China imesema inapokea parachichi kutoka Tanzania na imeahidi kuendelea kupokea mazao mengine hususan maharage ya soya.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Balozi wa China, Chen Mingjian, alipozungumza na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, kwenye ofisi ndogo ya Wizara jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali yake wakati wote imekuwa rafiki mzuri kwa Tanzania na uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo mbili unaendelea kuwa mzuri na unaimarika siku hadi siku.

"Kwa sasa China inapokea parachichi kutoka Tanzania na iko tayari kupokea mazao mengine hususani maharage ya soya kwenye soko lake, Watanzania wanakaribishwa kuleta bidhaa hizo China kwani soko la uhakika lipo," alisema.

Waziri Kijaji alisema Serikali ya Tanzania na ya China zimeahidi kuendeleza uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo kwa kuzingatia misingi ya uhusiano na ushirikiano wa kirafiki.

Alisema urafiki baina ya nchi hizo mbili ulianza mwaka 1961 na watauendeleza ili kuenzi mazuri yaliyofanywa na waasisi wa nchi zote mbili walioanzisha uhusiano huo.

Dk. Kijaji alisema Tanzania iko tayari kuwawezesha wafanyabiashara wa pande zote mbili, kushirikiana na kufanya biashara zao ili kuongeza ajira na kukuza uchumi wa wananchi wa mataifa hayo.

Waziri Kijaji na balozi huyo pia walijadiliana kuhusu namna ya kuenzi reli ya TAZARA na kufufua Kiwanda cha Urafiki ambacho ni matunda ya uhusiano baina ya nchi hizo pamoja na mikakati mbalimbali ya kuendeleza biashara.



Rose Njilo wa Shirika la MUMITIE linalopigania haki za watoto, wasichana na wanawake katika jamii ya Kimasai, akichangia mada kwenye kongamano la maadhimisho ya miaka 15 ya Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), lililofanyika Chuo Kikuu Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bil. 100/- kujenga vyuo vya VETA 63

Na Restuta James

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imesema zaidi ya Sh. bilioni 100 zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi zilizopelekwa kwenye wilaya 63.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Ofisa Habari wa VETA, Dora Tesha, alisema ujenzi wa vyuo unaendelea kwenye wilaya ambazo hazikuwa na vyuo hivyo.

Alizitaja kuwa ni Arumeru, Ubungo, Kinondoni, Chamwino, Kondoa, Mpwapwa, Bukombe, Mbogwe, Nyang'hwale, Kilolo, Mufindi, Biharamulo, Ngara, Kyerwa, Misenyi, Mlele, Tanganyika, Kakonko, Kibondo, Hai, Siha, Mwanga, Rombo, Same, Kilwa, Liwale, Nachingwea, Hanang, Kiteto, Mbulu, Bunda na Tarime.

Nyingine ni Rorya, Serengeti, Gairo, Kilombero, Malinyi, Tandahimba, Nanyumbu, Sengerema, Magu, Misungwi, Njombe, Bagamoyo, Kibiti, Mkuranga, Kisarawe, Kalambo, Mbinga, Tunduru, Kahama, Maswa, Meatu, Busega, Manyoni, Mkalama, Iramba, Songwe, Momba, Sikonge, Nzega, Muheza na Handeni.

Alisema kiasi hicho cha fedha pia kimeelekezwa kujenga chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe.

Alisema serikali imekusudia kujenga vyuo hivyo nchi nzima ikiwa ni azma yake ya kuzalisha ajira kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ufundi mbalimbali ikiwamo utaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ufundi vipuri, umeme, makenika, uchomeleaji, ufundi bomba viwandani na majumbani.

# Kampuni za kibiashara kuwania tuzo za SDG

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la UN Global Compact Network Tanzania limezindua mchakato wa kutafuta mshindi wa tuzo zitakazokuwa zinatolewa kila mwaka kwa kampuni za kibiashara zilizoonyesha kwa vitendo mchango wake kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Mchakato huo ulizinduliwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Shaban, kwa lengo la kuendeleza ushirikiano kati ya wadau wa sekta binafsi na serikali katika utekelezaji malengo ya maendeleo endelevu.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema UN Global Compact chapa ya Tanzania ambayo inajumuisha wadau wa sekta binafsi, ni washirika muhimu wa serikali ambao hufanya mapitio ya hiari ya malengo hayo ya maendeleo endelevu. "Mathalani, mwaka 2019 Tanzania ilikwenda kutoa utekelezaji wake wa malengo na mwaka 2023 Tanzania inakwenda kutoa tena, hivyo lazima ishirikiane na wadau mbalimbali na moja ya wadau muhimu ni sekta binafsi ambao wanatusaidia utekelezaji wake.

"Wadau hawa tumewaomba waangalie hii tuzo ya kibiashara inaweza vipi kusaidia utekelezaji malengo yetu ya kitaifa lakini haya malengo yamejumuisha malengo ya maendeleo endelevu, hii ni katika kubadilisha ulimwengu ni katika kutekeleza hayo, ndio kuna ajenda 2030," alisema.

Alisema Serikali ya Tanzania imechagua maeneo matano ambayo ni muhimu. Maeneo hayo ni watu, dunia, ustawi wa watu, usalama na ubia ambao unalenga kuendeleza ushirikiano kati ya serikali na wadau wa sekta binafsi. Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la UN Global Compact Network Tanzania, Simon Shayo, alisema tuzo hizo zinalenga kutathmini malengo 17 ya maendeleo endelevu ambayo Taifa hujipima kila mwaka.

Shayo ambaye ni Makamu Rais wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) anayeshughulikia maendeleo endelevu kwa upande wa Tanzania na Ghana, alisema licha ya kwamba ulimwengu utapimwa ifikapo mwaka 2030 kuona nchi zimefikia wapi kwenye maendeleo hayo, kubwa linalokalopimwa ni ubia.

Alisema lengo la 17 linaitaka serikali na wadau sekta binafsi na wengine kuingia kwenye ubia wa pamoja katika kuhakikisha kwamba maendeleo yanayofanyika sasa, yanasaidia kuhakikisha kwamba hakuna makundi au nchi zinazobaki nyuma.

"Malengo ya Maendeleo yetu yatakapofika 2030 tunataka tuone uwazi, kupungua kwa umaskini na uboreshaji wa maisha ya watu duniani pote.

"Tuna maeneo ambayo serikali imeshirikiana na sekta binafsi na serikali imechagua malengo matano ambayo itajipima kuonyesha pia nini mchango wa sekta binafsi kufikia malengo haya.

"Kwa hiyo, malengo mengi kama mnavyoona kwenye mpango wa taifa wa maendeleo na kwenye mpango wa 2025 serikali inafanya vizuri, licha ya kwamba yapo maeneo ambayo tulichelewesha na madhara ya janga la UVIKO-19 lakini kama nchi na wadau wake tuna hatua ambazo tumechukua kuhakikisha kwamba tunapiga hatua," alisema.

Aliongeza kuwa maeneo hayo ambayo Taifa limepiga hatua ni elimu, maji na maeneo mengine wanaamini kufikia 2030 kama nchi inayoendelea itakuwa imepiga hatua kubwa.

Alisema kitendo cha wadau wa sekta binafsi kukutana na serikali kufanya mapitio ya taarifa ya pamoja ni uthibitisho kwamba kuna ushirikiano mzuri.

"Mfano, miradi yote ya maji utekelezaji wake unaandaliwa na kuathiriwa na serikali, sekta binafsi pia na wadau wa maendeleo," alisema na kusisitiza kuwa hilo ni moja ya maeneo ambayo serikali imeonyesha kupiga hatua kubwa.

"Lakini katika suala la usawa wa kijinsia kama nchi tumepiga hatua kubwa, ukiondoa suala la asilimia 50/50 utaona hata kwenye miradi ya maendeleo tumegusa watu wote bila kumwacha mtu pembezoni.

"Hivyo, kama sekta binafsi tunayo nafasi kuendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kwamba kila moja katika malengo haya lile la 16 na 17 la ubia tunapiga hatua," alisema.

Alisema UN Global Compact ingependa kampuni za kibiashara zitazame mwenendo wao ili lengo lisiwe faida pekee bali iwe faida endelevu kwa maana kwamba faida ya kampuni na biashara zake zionekana kugusa watu.

"Pia zionekane kulinda dunia na vizazi vijavyo, zionekane kuleta ustawi kwa watu wote, zionekane ni biashara zinazojenga ubia na serikali na mwisho tunaamini biashara na serikali zitaleta maendeleo," alisema Shayo.

Mbali na tuzo hizo, alisisitiza kuendeleza kuwapo mijadala kuhusu taarifa ya hiari ambayo Tanzania ni moja ya nchi 42 ambazo zitatoa taarifa kwa hiari kuonyesha wamefikia wapi kwenye utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu itakapofanyika Julai mwaka huu nchini Marekani.

Mjumbe wa Shirika hilo la UN Global Compact chapa ya Tanzania, Anna Henga, alisema kuwapo kwa chapa hiyo kunalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu uwekezaji na watu wanaopokea wawekezaji.

Alitolea mfano wa changamoto hizo kuwa ni masuala ya fidia kwa watu wanaofikiwa na uwekezaji, kodi kwa kampuni zinazowekezaji pamoja na malalamiko mengine.



## Miundombinu ujenzi bomba la mafuta yaanza kujengwa

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

UJENZI wa awali wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), umeanza rasmi katika eneo la Chongoleani, mkoani Tanga, baada ya kampuni inayotekeleza mradi huo, kuandaa eneo ujenzi wa matangi, jeti, miundombinu ya bandari na makazi ya muda ya wafanyakazi.

Inakadiriwa mapipa 216,000 ya mafuta ghafi, yatasafirishwa kwenye bomba hilo kwa siku moja kutoka Uganda kwenda kwenye Peninsula ya Chongoleani nchini Tanzania, ambako yatajengwa matangi ya kuhifadhia mafuta, kabla ya kupakiwa kwenye meli na kwenda kuuzwa katika soko la dunia.

Mkurugenzi wa Petroli wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Gerald Maganga, alisema serikali ya Tanzania, inaridhishwa na hatua za awali za uandaaji wa utekelezaji wa mradi huo mkubwa.

Maganga, alikuwa akizungumza jana na ujumbe wa maofisa wa Mamlaka ya Petroli ya nchini Uganda (PAU), walioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Ernest Rubondo, baada ya kutembelea na kukagua hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo.

"Tumeona maeneo mbalimbali yakiandaliwa kwa ajili ya kujenga matangi na miundombinu mingine. Tumefurahishwa hasa na namna wanavyozingatia ushirikishwaji wa wazawa katika kufanya kazi mbalimbali.

"Kazi inaridhisha na inakwenda vizuri. Matumaini yetu ni kwamba muda uliopangwa kukamilisha ujenzi huo utakwenda sawa kama ilivyotarajiwa,"alisema Maganga.

Kutokana na umuhimu wa mradi huo, mkurugenzi huyo, amewashauri Watanzania wakiwamo watoa huduma za ukandarasi, kujiandikisha kwenye kanzidata ya EWURA ili kupata fursa ya kunufaika na kazi mbalimbali za utoaji wa huduma, wakati wa ujenzi wa mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Petroli ya Uganda (PAU), Ernest Rubondo, alipongeza hatua iliyofikiwa, huku akieleza matumaini yake katika maendeleo ya ujenzi wa bomba hilo la mafuta ghafi la Afrika Mashariki.

# Mkenda aipa 'tano' AKO kuwekeza kwenye elimu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, ameeleza kufurahishwa na uamuzi wa Shirika la AKO Tanzania Community Support, kuwekeza Sh. milioni 840 kwenye ukarabati na ujenzi wa miundominu ya shule za msingi.

Shirika hilo linatekeleza miradi mipya ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya sekta ya elimu katika Wilaya ya Hai na Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Kwa kweli ni faraja kwetu kama serikali na hasa watu wa Moshi Vijijini na Hai. Tunalishukuru shirika hili kwa jicho lake la kuona uchakavu wa vyumba vya madarasa, ofisi za walimu, jicho na miundombinu mingine ya vyoo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Hilda Kimathi, alisema katika Wilaya ya Hai, miradi mipya ya ujenzi inaihusisha Shule Jumuishi ya Wenye Ulemavu inayojengwa Shule ya Msingi Kibaoni, inayojengwa kwa Sh. milioni 100 na Shule ya Msingi Darajani, inakotekeleza mradi wa ujenzi vyumba viwili vya madarasa, choo cha wanafunzi na walimu na ofisi ya walimu, kwa Sh. milioni 150.

Miradi mingine ni ya ujenzi wa jiko la kisasa, vyumba vya madarasa na ofisi za walimu katika Shule ya Msingi Uchau iliyoko Moshi Vijijini ambao utagharimu Sh. milioni 240.

Miradi inayotekelezwa eneo la Moshi Vijijini inagharimu Sh. milioni 590 na miradi mipya miwili inayotekelezwa katika Wilaya ya Hai itagharimu Sh. milioni 250.

"Miongoni mwa sababu ambazo zimetusukuma AKO Tanzania Community Support, kujitosa kutekeleza miradi hii ya elimu ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na kukosekana kwa kwa miundombinu rafiki katika shule zetu. Jambo ambalo tunaona limekuwa likichangia kushuka kwa kiwango cha elimu nchini.

"Shule nyingi za serikali zinatishiwa na uchakavu wa miundombinu yake, ndio maana tumeamua kuweka mkono wetu kuiunga serikali na kuwatua mzigo wa kuchangia gharama za ukarabati wananchi wa maeneo hayo yatakayonufaika." Alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, miradi mingine ambayo inatekelezwa na AKO Tanzania Community Support katika eneo la Moshi Vijijini ni ukarabati wa shule tatu chakavu za msingi, zilizokuwa zikihatarisha maisha ya wanafunzi na walimu kutokana na vyumba vya madarasa kukatika nyufa na kuharibika vibaya miundombinu yake.

Aidha, imo miradi ya Sh. milioni 350 ambayo inazihusisha Shule ya Msingi Sungu, Shule ya Msingi Kibosho na Shule ya Msingi Singachini.

Vilevile, AKO Tanzania Community Support, inatekeleza mradi wa ukarabati wa Shule ya Msingi Sungu (Sh. milioni 100), Shule ya Msingi Kibosho (Sh. milioni 50) na Shule ya Msingi Singachini (Sh. milioni 200). Akizungumzia miradi hiyo, namna inavyowasaidia kurejesha hamasa ya ongezeko la ufaulu, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uchau, Agness Mbwambo, alisema: "Tumepata mradi kutoka Shirika la AKO Tanzania Community Support, wametujengea jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na walimu. Kabla ya mradi huu, chakula kilikuwa kikipikwa katika vyumba vya madarasa."

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Hans Simmer, alisema AKO Tanzania Community Support, imejikita kusaidiana na jamii, kukarabati shule za msingi ambazo hali ya majengo yake ni mbaya ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.




Baadhi ya wafanyakazi wa mgodi wa Barrick North Mara, wilayani Tarime wakifurahi baada ya kumaliza kukimbia katika mbio za kimataifa za Kilimanjaro Marathon zilizofanyika mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi 200,000 wajumuishwa mpango wa kinga tiba usubi

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI zaidi ya 202,000 wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wamejumuishwa katika mpango wa Wizara ya Afya wa matumizi ya kinga tiba ya ugonjwa wa usubi kwa mwaka huu. Serikali inatekeleza mpango huo ili kufikia malengo yake ya kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele, wilayani humo, Julius Mgeni, alidokeza kuhusu walengwa hao jana, wakati wa kikao cha tathmini na upangaji mikakati ya umezaji dawa hizo. "Ugonjwa huu huenezwa na nzi wadogo weusi, ambao kitaalamu wanaitwa blackfriars, ambao huzaliana katika maeneo yenye misitu na maji yanayotiririka kwa kasi," alisema.

Ugonjwa wa usubi, unaathiri ngozi ya binadamu na miongoni mwa dalili zake ni kupatwa na homa kali, kutokwa na vipele mwilini, kuhisi muwasho mkali na wakati mwingine unaweza kusababisha upofu.


Mgeni alisema kuwa Halmashauri ya Wilaya hiyo, imelenga kuwafikia wananchi 202,203 mwaka huu.

Utekelezaji wa mpango huo, umepangwa kuanza kutekelezwa Machi 3 hadi Machi 7 mwaka huu na litafanyika katika vituo vyote vilivyopangwa.

Aidha, Mratibu wa Afya Shuleni wa Wilaya hiyo, Ibrahimu Kombo, alisema katika utekelezaji wa mpango huo, idadi ya wanafunzi walioandikishwa, wasichana ni 23, 584, wavulana ni 23, 729, sawa na wanafunzi 47,313.

Akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Japhet Haule, aliwaagiza wasimamizi wa mpango huo, kuwateua watoa huduma ya afya ngazi ya jamii wanaokubalika ili kuongeza nguvu ya kuishawishi jamii kupata kinga tiba hizo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Cyprian Mselem, aliwasihi baadhi ya wananchi wanaopotosha mpango wa utoaji wa dawa hizo, kuacha propaganda hiyo, kwa kuwa unaivuruga serikali katika mipango yake ya kuwakinga wananchi wake na magonjwa hayo tishio.





# Baba ashikiliwa tuhuma kulawiti watoto wake

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia, Haule Abel (38), mkazi wa Ngokolo Manispaa ya Shinyanga kwa tuhuma za kulawiti watoto wake wawili (majina yamehifadhiwa).

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ofisini kwake na kusema watoto hao mmoja ana miaka nane na mwingine 11.

Alisema tukio hilo lilitokea Februari 21, mwaka huu majira ya saa 4 usiku na kwamba mtuhumiwa huyo amekuwa akiwafanyia mchezo huo watoto wake kwa muda mrefu.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tunamshikilia baba kwa tuhuma za kulawiti watoto wake wawili mmoja akiwa na miaka minane na mwingine 11 na kesi hii mimi mwenyewe naisimamia na jarada tayari tumelipeleka kwa mwanasheria na tutamfikisha mahakamani," alisema Magomi.

Katika hatua nyingine Kamanda Magomi alikemea tabia ya baadhi ya askari wasio waadilifu wanaotoa siri kuhusu taarifa wanazopewa na wananchi kuhusu uhalifu na wahalifu.

Akizungumzia msako waliofanya hivi karibuni alisema jeshi hilo limefanikiwa kukamata mafuta ya dizeli lita 780 yaliyoibwa kwenye Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) pamoja na pikipiki tatu ambazo zilikuwa zikitumika katika wizi huo.

Alitaja vitu vingine vya wizi ambavyo wamevikamata kuwa ni milango ya chuma, mabomba ya alama za usalama barabarani, milango mitano ya mbao, mizani ya kupimia uzito, mashine ya kutoboa miamba, godoro moja, viti vinne vya plastiki, ngoma moja ya shule na magitaa mawili, vifaa tiba na mashine mbili za kamari.

Vingine ni pamoja na redio mbili, feni moja, mtungi mmoja wa gesi.

Alisema katika msako huo pia waliokota pikipiki mbili, huku akibainisha kuwa wamekamata pia bangi misokoto 31, waganga wa jadi watatu wakiwa na vifaa vya kupigia ramli chonganishi ambavyo husababisha mauaji ya kikatili.



Mbunge wa Jimbo la Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Ilamba, Kata ya Igwamanoni Halmashauri ya Ushetu, kwenye maadhimisho ya uongozi wa mwaka mmoja tangu alipochaguliwa jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mbaroni kwa kuwamwagia maji ya moto mama na mtoto

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

MKAZI wa Shunu, Kata ya Nyahanga Manispaa ya Kahama, Marysiana Thomas (21) pamoja na mtoto wake wamemwagiwa maji ya moto na rafiki yake sehemu za kifuani na tumboni.

Kisa hicho kilitokea baada ya Merysiana kupigiwa simu na mume wa rafiki yake aliyemtaja kwa jina moja la Zabela baada ya kutopatikana kwenye simu yake.

Merysiana alisema yeye ni mpangaji kwenye familia ya mume wa rafiki yake na kwamba baba mwenye nyumba hiyo humpigia simu mara kwa mara pindi akihitaji kuongea na mke wake, lakini siku hiyo alipiga simu mara ya kwanza akamwambia asubiri wakati huo alikuwa akipika mboga akiogopa itaungua alivyopiga mara ya pili akampelekea rafiki yake lakini hakuichukua simu hiyo.

"Mimi nikamweleza ni mume wako anakutafuta chukua uongee naye, akaniambia umezoea anakupigia simu wewe kama nani? Nikajua utani baada ya hapo alinimwagia maji, alisema.

Alisema huwa mara nyingi wanaazimana simu na kuongea kama mmojawapo hana salio la kupiga simu au intaneti, lakini siku hiyo rafiki yake aligeuka na kumwagia maji yaliyokuwa jikoni kwa ajili ya kusonga ugali.

Mama mkwe wa rafiki yake, Amina Daniel ambaye anayemhudumia hospitalini kwa ajili ya kupata matibabu alisema kitendo hicho kimemsikitisha na kwamba hakufikiria kama ingetokea hali hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Philipo Nyaga, alisema mama huyo na mtoto wake waliunguzwa na maji ya moto sehemu mbalimbali za miili yao na wameanza kupata huduma na hali zao zinaendelea vizuri.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mtuhumiwa amekamatwa.

## Mradi wa maji uliokwama kwa miaka 10 wakamilika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MRADI wa maji uliodumu kwa miaka 10 katika Kata ya Sabasabini Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga umekamilika na kuanza kutoa maji kwa wananchi.

Diwani wa kata hiyo, Emmanuel Makashi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Ilamba kwenye mkutano wa wananchi.

Makashi alisema mradi huo ulianza ujenzi mwaka 2013, lakini ulishindwa kukamilika kwa wakati baada ya kukosekana kwa fedha za ukamilishaji na kusababisha wananchi kukosa matumaini ya kupata huduma hiyo.

Alisema Oktoba 10, mwaka jana kulifanyika mkutano wa hadhara katika kata hiyo na wananchi wakatoa kero zao ikiwamo kukosa majisafi na salama kwenye eneo lao.

Aliongeza kuwa kitendo cha kukamilika mradi huo uliodumu kwa kipindi cha miaka 10, umesababisha wananchi hao kumpongeza mbunge wao.

"Wananchi wa kata hii ilikuwa inatumia maji ya kwenye visima vifupi vilivyochimbwa jirani na makazi yao na katika madimbwi ya maji yaliyochimbwa kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao na kipindi cha kiangazi yalikauka, lakini kwa sasa hali hiyo haipo tena baada ya mradi huu kukamilika na kutoa huduma," alisema Makashi.

Mkazi wa kata hiyo, Ferister Kabasa, alisema awali kabla ya mradi huo kukamilika walitumia maji yasiyokuwa safi na salama na magonjwa ya mlipuko kama vile kichocho na kuumwa matumbo hususani kwa watoto wadogo yalikuwa mengi ikilinganishwa na hivi sasa.

Mwananchi mwingine, Mponeja Bundala, alidai kuwa ndoa nyingi zilivunjika baada ya wake zao kuamka alfajiri kwenda kutafuta maji na kurejea nyumbani majira ya saa 7.00 mchana na wakati mwingine jioni hali ambayo iliwafanya kuingiwa na hofu ya kusalitiwa.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema, katika uongozi wake amejikita katika kutatua kero mbalimbali zinazowagusa wananchi moja kwa moja hususani katika sekta ya afya, maji, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara.

Alisema hivi karibuni kata 11 kati ya 20 za Ushetu zitapata huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria na wataalamu wapo kazini kwa ajili ya kuweka alama sehemu ambazo bomba litapita.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 28, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12



UNFPA, WiLDAF yawa mkombozi mabinti waliokatishwa masomo

Ukurasa 13



Wadau wanaokereka waja juu, sheria ifute adhabu hiyo inayowaumiza wanafunzi

Ukurasa 14



## Waunda shirika, wapiga hodi nyumba kwa nyumba kudai haki, ulinzi wao kisheria

ELIMU

**NA WAANDISHI WETU**

# Ndiyo au hapana kwa viboko shuleni, si uamuzi unaopatikana kwa urahisi

BAADHI ya watoto wakirejea nyumbani wana alama au michirizi mgongoni, kwenye makalio na hata mapajani. Wapo wanaotembea kwa taabu wakiulizwa shida ni nini jawabu limekuwa kupigwa idadi kubwa ya viboko tena kwa hasira na walimu shuleni.

Ni mjadala unaogusa maeneo mbalimbali kuhusu adhabu ya viboko, umefika hadi bungeni na kutolewa matamko.

Hadi leo adhabu ya viboko kwa wanafunzi shuleni ni suala lenye kufikirisha hasa ikichukuliwa kuwa kuna dhana kubwa mbili, mosi ni mnyama au punda bila mjeledi haendi kwa hivyo pia wanafunzi bila viboko hawawezi kufundishika hivyo kufikiri kuwa kuchapa kuendelee kwa manufaa ya wanafunzi.

Mtazamo wa pili ni kuwa viboko sio muhimu kwa wanafunzi na kunawaondolea hali ya kujiamini na pia hadhi ya utu wao inaondoka hivyo, viboko ni adui wa maendeleo na mafanikio ya mwanafunzi.

Ikumbukwe kuwa Tanzania, viboko shuleni vinasimamiwa na waraka wa Wizara ya Elimu namba 24 wa mwaka 2002 ambao unaelekeza idadi ya viboko, anayeruhusiwa kuadhibu, makosa yanayostahili adhabu hiyo na taratibu.

Februari mwaka huu Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anajibu hoja bungeni kuhusu adhabu ya viboko shuleni, akiahidi kushirikisha wadau katika suala hilo.



Adhabu hii ina maswali mengi, kama ni kufundisha au kuumiza? Inasaidia au inakomoa?. **PICHA: MTANDAO**

**MTIZAMO KIMATIBABU**

Mtazamo wa maadili ya sayansi na tiba (bioethics) kuhusu adhabu ya viboko shuleni, unaotolewa na wataalamu wa maadili duniani, unatazamwa kwa athari au matokeo ya adhabu hiyo.

Hizi ni nadharia ambazo zinazingatia matokeo ya kitendo hicho kilichofanyika ili kujua uhalali au uharamu wake. Mwanafalsafa wa Uingereza Jeremy Benthum, anaeleza kwamba “kuchapwa viboko kutakuwa sahihi ikiwa kutaleta furaha zaidi kuliko maumivu”.

Kwa mtazamo wa nadharia hizi, kitendo sahihi ni kile kinacholeta matokeo yenye faida kubwa zaidi kuliko hasara kwa wote wanaohusika ni kibaya ikiwa kitaleta matokeo ya hasara zaidi kuliko faida kwa wote wanaohusika.

Kwa mtazamo huo, ni muhimu kujua kati ya maumivu ya viboko na furaha inayotokana na viboko hivyo kipi kinazidi kingine. Kama imegundulika kwamba kumchapa mwanafunzi kunamfanya asome kwa bidii zaidi na afaulu mitihani yake, basi faida ya kuchapwa viboko itakuwa kubwa kuliko maumivu.

Kwa hiyo tendo la kumchapa mwanafunzi litakuwa sahihi kwa sababu linaleta maumivu kidogo na furaha kwa mwanafunzi mwenyewe, wazazi, walezi, ndugu na wote wanaopenda ufaulu wa mwanafunzi huyo.

Mwalimu pia ni mlezi mwenye wajibu wa kufundisha nidhamu na uwajibikaji kwa mwanafunzi, kwa mfano ikiwa viboko vitamfanya mwanafunzi kuwa msafi wa mwili na mazingira yake, ataepushwa na magonjwa na kwa hiyo viboko hivyo vitaleta furaha zaidi kuliko maumivu, hivyo kuwa halali.

Lakini, ikiwa mwanafunzi atachapwa na viboko vikamfanya awe na hofu kwa walimu kiasi cha kushindwa kuelewa masomo darasani na mwisho kufeli mitihani fimbo zitakuwa si sahihi na ni kinyume na maadili.

**NINI KIFANYIKE**

Wizara ya Elimu iko sahihi kimaadili ikiwa ilichunguza na kujiridhisha kwamba viboko shuleni vina faida zaidi kuliko maumivu, ikaandaa waraka namba 24 wa mwaka 2002.

Ni wazi itakapogundulika kwamba vinaleta madhara zaidi kuliko faida, vitakuwa ni kinyume na maadili na itakuwa ni bora kufuta adhabu hiyo.

Kwa upande mwingine, ikiwa fimbo zitaendelea kuruhusiwa shuleni, ni muhimu kwa wahusika wa kutoa adhabu hiyo kuzingatia nadharia nyingine iitwayo nadharia ya wajibu.

Kiingereza huitwa ‘duty theory’, hizi ni nadharia ambazo usahihi wa tendo haupimwi kwa kuangalia matokeo ya kitendo kilichofanyika bali wajibu wa kitendo chenyewe.

Kama tendo ni baya litabaki kuwa baya hata kama litaleta matokeo mazuri ya furaha katika jamii na litakuwa sahihi ikiwa linafuata sheria na kanuni zilizowekwa.

Katika kanuni za nadharia za matendo, mwanafalsafa Emmanuel Kant, anaelezea katika moja ya kanuni zake ambayo kwa kifupi zinaitwa za kuheshimu ubinadamu. Kwenye kanuni hii, Kant anasema.

“Fanya jambo kwa namna ambayo utaheshimu ubinadamu wako au wa mtu mwingine, sio kama njia ya kufanikisha jambo bali ubinadamu liwe lengo la mwisho kwa muhusika”.

Binadamu asitumike kama kifaa cha kufanikisha jambo bali matendo yanapaswa kuwa na lengo la kulinda ubinadamu wa kila mtu anayehusika katika kitendo hicho.

Kwa mtazamo huu, viboko kwa mwanafunzi vinapaswa kuheshimu ubinadamu yaani asichapwe kama anavyopigwa mnyama. Pia viboko hivyo vinapaswa kulenga manufaa ya mwanafunzi mwenyewe kwanza na isiwe ni njia ya kumnufaisha mwalimu au shule.

Kwa mfano, mwalimu anawachapa wanafunzi wote darasani kwa sababu wanapiga kelele na kuleta usumbufu shule nzima.

Hii ni kinyume na maadili kwa sababu inafahamika kwamba watoto watapiga kelele kukiwa hakuna mwalimu na wakiwa wengi darasani.

Ikiwa mwalimu hajatimiza wajibu wake wa kuwahi na kuwa darasani na ndiye anayetaka watoto wasipige kelele wakati hayupo, akija kuwachapa atafanya hivyo kwa kutanguliza malengo yake kwanza sio kwa faida ya wanafunzi.

**UMUHIMU WA VIBOKO**

Umuhimu wa adhabu na madhara yake kwa mwanafunzi

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, KISHAPU

# UNFPA, WiLDAF yawa mkombozi mabinti waliokatishwa masomo



Wanufaika wa mpango wa kuwasaidia wasichana waliopata changamoto za kielimu wakiwa kwenye hafla ya kutambulishwa na kukabidhiwa kwa uongozi wa vyuo vya VETA Kishapu, Kahama na Shinyanga: **PICHA: MARCO MADUHU**

MIKOA ya Shinyanga pamoja na Mara ni tatu bora za mimba na ndoa za utotoni kwa mabinti walio chini ya umri wa miaka 18.

Ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2012 na Shirika la Watoto Duniani (UNICEF), kwamba Shinyanga ina asilimia 59, Tabora 58 na ya tatu ni Mara kwa asilimia 55.

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (Women in Law and Development in Africa WiLDAF), limeanzisha mikakati ya kuwasaidia mabinti hao.

WiLDAF ina programu ya chaguo langu haki yangu, ambayo lengo lake ni kuwanyanyua tena mabinti waliopata watoto katika umri mdogo pamoja na vijana wa riki linalopevuka kwa kuwasomesha katika vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) ili wapate ujuzi na kutimiza ndoto zao na kumudu maisha yao.

Rehema Maro ni Mkuu wa Programu wa WiLDAF, anasema wamewatafuta mabinti 290 kutoka Kahama na Kishapu za mkoani Shinyanga, pamoja na Butiama mkoani Mara, ambao baadhi wamepata watoto wakiwa wadogo na wengine rika balehe wakishindwa kuendelea na masomo na kubaki bila msaada.

Rehema anasema wanaguswa na tatizo la mimba na ndoa za utotoni katika mikoa hiyo na sasa mabinti wameanza kusoma mafunzo ya ufundi Februari mwaka huu katika vyuo vya VETA Kahama, Shinyanga na Kishapu.

Anasema WiLDAF inawagharamia kila kitu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Finland na siku ya kuhitimu mafunzo yao watapewa vitendea kazi na mitaji ili wakajiajiri na kuendesha maisha yao.

"Tumedhamiria kurudisha matumaini kwa mabinti ambao walijifungua katika umri mdogo na kuacha masomo, tunawasomesha bure mafunzo ya ufundi ili wapate ujuzi na kutimiza ndoto zao na kuacha kuwa tegemezi, bali watafanya shughuli zao na kujiingizia kipato," anasema Rehema. "Mafunzo yatakuwa endelevu na mabinti watakuwa wakisoma kwa awamu. Tunachokiomba kwa wazazi na walezi wasifiche mabinti hasa wale wenye ulemavu, sababu kipindi tunawatafuta tulipata shida kuwapata wenye ulemavu," anaongeza.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kishapu, Joseph Swalala, anasema mabinti hao wamepata nafasi ya kipekee sababu walikuwa hawasomi tena na wamegeuka kuwa mama wa familia, lakini sasa wanasaidiwa kupata ujuzi.

Anasema tatizo la mabinti kukatishwa masomo sababu ya mimba na ndoa bado lipo licha ya serikali na wadau kuendelea kulipigia kelele na kulikemea, lakini jamii imekuwa vigumu kubadilika na kuendelea kuzima ndoto za wanafunzi.

"Fursa ambayo mmeipata itumieni kikamilifu msiipoteze someni kwa bidii na kupata ujuzi ambao utatimiza ndoto zenu na kujikomboa kimaisha,"anasema Swalala.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga Dafroza Ndalichako, akiwa kwenye kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa Februari mwaka huu, anataja takwimu za wanafunzi ambao wamepewa mimba na kuacha masomo mwaka jana mkoani humo kuwa ni 147 shule za msingi mimba 28 na sekondari 119.

Prisla Mushi ni Ofisa Ustawi wa Jamii Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, anayesema jamii kuendekeza vitendo vya kufanya ngono na watoto ni makosa kisheria na kuwataka mabinti hao wasijihusishe tena ili wasikwame wakiwa masomoni VETA na kuharibu kabisa dira ya maisha yao.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 mtoto ana haki ya kupewa ulinzi, elimu na mahitaji yote ya msingi, hivyo kisheria ni hatia kuwashirikisha kwenye ngono.

Ofisa Elimu Sekondari wilayani Kishapu, David Mashauri, anawasihi mabinti hao wayazingatie mafunzo ambayo watayapata katika vyuo hivyo vya ufundi, ambayo yatakuwa na manufaa katika maisha yao kwa kujiajiri wenyewe na kuanza ukurasa mpya wa maisha.

Mkuu wa Chuo cha VETA mkoani Shinyaga, Mangu Mabelele, ambaye anasimamia pia Chuo cha VETA wilayani Kishapu, anawakaribisha akiwaambia ufundi stadi kwa sasa ndiyo habari ya mjini sababu mtu mwenye ujuzi hawezi kushinda njaa.

Anasema Shirika la WiLDAF kuamua kuwapatia ujuzi mabinti hao hawajakosea bali wamewapeleka mahali sahihi sababu mwenye ujuzi hana haja ya kulilia kuajiriwa bali anauwezo wa kujiajiri mwenyewe na kuendesha maisha yake.

"Sisi VETA tupo tayari kuwafundisha mabinti hawa fani mbalimbali ambazo watazichagua zikiwamo za ushonaji nguo, urembo na mapambo, ususi, ufundi mabomba, uendeshaji wa mitambo, uchomeleaji yaani fani zipo nyingi ambazo zitawasaidia katika maisha yenu," anasema Mabelele.

Ester Jovani kutoka wilayani Kishapu ambaye ana mtoto mmoja, anaahidi kusonga mbele na si kurudia makosa.

Kadhalika Naomi Jonas kutoka Butiama mkoani Mara, anasema ujuzi ambao ataupata kutoka VETA kwenye ufundi wa kushona nguo, atakwenda kuanzisha ofisi yake nyumbani kwao na kuacha kuwa tegemezi kwa wazazi wake, bali yeye atageuka kuwa msaada kwao.

## Ndiyo au hapana kwa viboko shuleni, si uamuzi unaopatikana kwa urahisi

**INATOKA UK.11**

ni jambo la kutambua kwamba kuna wakati mwanafunzi hastahili kuchapwa hata kama akikosea, kumkemea kunaweza kumfanya ajirekebishe zaidi kuliko kumchapa.

Viboko vya mara kwa mara vinaweza kumtia hofu na kumfanya afeli mitihani. Lakini wakati mwingine huenda viboko vikawasaidia wanafunzi kujirekebisha na hasa pale wanaporudia mara kwa mara kufanya makosa makubwa ya utovu wa nidhamu kama vile kupigana, wizi na kutumia lugha ya matusi kwa wanafunzi wenzao hata kwa walimu.

Kwa mtazamo huo, viboko vitakuwa sahihi kimaadili ikiwa vitalenga kumsaidia mwanafunzi mwenyewe kubadilika kwanza na vitalinda heshima na binadamu wake. Viboko visivyolenga kumsaidia mwanafunzi na vikawa vinashusha na kudhalilisha utu wake ni kinyume na maadili.

Wahusika wa maamuzi ya adhabu ya viboko wanapaswa kuwa na muda wa kutosha na uwezo wa kutambua ni wakati gani sahihi wa kutumia adhabu hiyo.

Ni muhimu pia kutambua tabia za wanafunzi na afya zao kabla ya kutumia adhabu hiyo. Kwani kuna mwanafunzi akiona mwalimu anakuja na kiboko hukosa utulivu wa akili na mwili na hivyo kumfanya asiweze tena kusoma wala kuelewa kipindi au masomo.

Lakini, kuna mwanafunzi akiona mwalimu amekuja na kiboko basi hujitahidi na kujituma kwa nguvu na akili zake zote ili afanye vizuri ili kuepuka viboko. Kwa mantiki hivyo ni wajibu wa walimu kumwelewa vizuri mwanafunzi wake na kutumia njia sahihi itakayofanya afanye vizuri katika masomo yake.

**USHAURI MUHIMU**

Cha msingi ni kwamba adhabu ya viboko ni suala lenye kuhitaji muda na ushiriki wa jamii mbalimbali. Kwa mantiki hivyo ni wajibu wa walimu kumwelewa vizuri mwanafunzi wake na kutumia njia sahihi itakayofanya afanye vizuri katika masomo yake na kuwa na madili mema katika jamii.

*Imeandikwa na Shabani Mkumbugo (0718-473499) na Pankras Luoga (0757-645746) kutoka MUHAS.*

ELIMU
NA ELIZABETH ZAYA

VIBOKO SHULENI

# Wadau wanaokereka waja juu, sheria ifute adhabu hiyo inayowaumiza wanafunzi

TAASISI ya HakiElimu inapendekeza kupitiwa upya vipengele vya mwongozo na sheria ya elimu kuhusu adhabu za viboko, ikigusia pia kuvigusa upya vipengele vya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na kuharamisha kuchapa viboko shuleni.

Kadhalika kuzuia adhabu nyingine ambazo zinatoa mwanya wa kufanyika ukatili kwa watoto shuleni, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu Dk. John Kalage, anasema.

Anaeleza kuwa kuna haja ya kuanzishwa programu ya shule salama katika shule zote 18,000 za msingi badala ya 600 pekee ambazo serikali imesema inaziweka chini ya mradi huo, kadhalika kuingiza katika miongozo na kanuni za uendeshaji wa shule.

Anapendekeza kuweka mipango endelevu ya kuimarisha mifumo rasmi ya ulinzi na usalama wa watoto shuleni ikiwa ni pamoja na kuharakisha kuanzishwa madawati ya ulinzi na usalama na mabaraza ya watoto.

Aidha, Dk. Kalage inaitaka serikali kutoa elimu kwa wanafunzi, shuleni, kwenye nyumba za ibada na maeneo ambayo watoto wanakusanyika, kuchukua hatua kali dhidi ya wanaobainika kuhusika na ukatili kwa watoto ili kuukomesha ndani na nje ya shule.

Mapendekezo mengine ni kuhakikisha mafunzo ya walimu yanahusisha moduli zinazohusu kutoa adhabu chanya na jinsi ya kurekebisha wanafunzi wenye matatizo ya tabia na mwenendo mbaya.

Anataja mafunzo tarajali ya walimu kuhusisha ngazi zote, kozi maalum za kuwafundisha watoto wenye matatizo ya mienendo mibaya na kutoa adhabu chanya.

Dk. Kalage katika mazungumzo yake anasema ni vema kuhakikisha miiko na maadili ya walimu inahuishwa ili kuwagusa hata wale wanaoshindwa kuzuia matendo ya kikatili kwa watoto yanayofanywa na walimu wenzao.

"Kwa mfano lile tukio la kuchapwa mwanafunzi mkoani Kagera, tuliona watoto walichapwa huku walimu wengine wakicheka. Katika mikasa mingine tumeona watoto wakichapwa walimu wakishuhudia, ni muhimu kuwahimiza watumike kuimarisha stadi zao za maisha na uwezo wa kukabiliana na changamoto za wanafunzi,"anasema Dk. Kalage.



Mwalimu akimwadhibu mwanafunzi shuleni. **PICHA MTANDAO**

Anasema taasisi yake inapendekeza kwamba, masomo yanayohusiana na maadili yafundishwe na walimu wenye uwezo ili kusaidia wanafunzi kukua kimaadili pamoja na ushirikiano kati ya wazazi na walimu ikiwamo kuweka bayana kikanuni wajibu wa walimu na wazazi kwa watoto.

HakiElimu inasema taarifa za hali ya ukatili nchini inayotolewa na Jeshi la Polisi, inaonyesha kuwa visa vya ukatili kwa watoto viliongezeka kwa asilimia 25.9 kutoka visa 5,803 ilivyoripotiwa mwaka 2015 hadi visa 7,388 mwaka 2020.

Mkurugenzi wa HakiElimu, anasema katika utafiti uliofanywa na taasisi hiyo mwaka 2020 ulionyesha kuwa asilimia 87.9 ya watoto wa shule waliripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili huku asilimia 90 kati ya hao ukitokana na adhabu za viboko zilizotolewa shuleni.

"Katika utafiti huu, asilimia 54.9 ya watoto wanataja walimu wao na walezi kuwapiga ngumi na makofi kama sehemu ya adhabu wanapokosea. Tanzania bado inakumbatia adhabu ya viboko kwa watoto shuleni,"anasema Dk. Kalage.

"Kwa mujibu wa mwongozo wa elimu kuhusu adhabu za viboko wa mwaka 2002, mwalimu mkuu anaruhusiwa kutandika viboko kwa wanafunzi au kukasimu jukumu hilo kwa mwalimu mwingine. Mwongozo huu unapewa nguvu na sheria ya elimu ya mwaka 1978 na mabadiliko ya 2002."

Anaeleza kwamba sheria hiyo kwenye kipengele cha 60, kinaruhusu kutolewa adhabu mbalimbali kama sehemu ya kuhimiza nidhamu kwa watoto.

Anasema pamoja na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ya Tanzania Bara kuzuia vitendo vya kutesa au vya kikatili kwa mtoto, lakini bado haitoi katazo la moja kwa moja kwa adhabu ya viboko kwa watoto.

"Pamoja na kuwa madhara ya adhabu yameelezwa kwenye mafunzo ya taaluma ya ualimu, ikiwamo maumivu ya aina mbalimbali kwa watoto, kujenga chuki na hata kupunguza motisha ya kujifunza au kwenda shule, bado sehemu kubwa ya walimu wanaona matumizi ya viboko ndio njia rahisi na yenye ufanisi katika kuhimiza watoto kujifunza kwa bidii," anasema.

Anasema walimu wanasisitizwa kutumia mbinu mbadala katika kusimamia nidhamu ya wanafunzi ikiwamo vichocheo hasi ili wanafunzi wasiendelee na mienendo ambayo haifai badala ya adhabu ikiwamo viboko.

Kalage anasema matumizi ya njia mbadala kusimamia nidhamu yanategemea sana uwezo wa walimu katika kuzitumia.

"Kinachojitokeza wazi ni kwamba, walimu wengi wanashindwa kutumia njia mbadala na kwa kuwa sheria na miongozo inaruhusu viboko, basi wanachagua hiyo.

Anatoa wito kwa serikali kuchukua hatua ambazo zitakomesha matumizi ya adhabu za viboko shuleni na kuhimiza nyingine chanya au mbadala ambazo sio za kikatili.

"Ni rai yetu vipengele vya sheria ya elimu ya mwaka 1978, mwongozo wa elimu wa adhabu za viboko wa mwaka 2002 na sheria ya mtoto ya mwaka 2009, vipitiwe upya ili kukataza kabisa adhabu za viboko shuleni na kuzuia adhabu nyinginezo ambazo zinatoa mwanya wa ukatili kwa watoto kufanyika,"anasema Kalage.

Hivi karibuni kumekuwa matukio ya walimu kuwaadhibu wanafunzi kwa viboko kiasi cha kuwasababishia madhara kimwili na kisaikolojia na hata wengine kufariki dunia.

Adhabu, hizi zimekuwa zikitolewa na walimu bila kuzingatia miongozo ya kanuni na sheria dhidi ya makosa mbalimbali zilizowekwa na serikali na sheria, na hivyo kusababisha madhara makubwa si tu kwa watoto pekee bali wazazi na uongozi wa shule kwa ujumla.

Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na lile lililotokea katika Shule ya Msingi Kahanja Kyerwa mkoani Kagera, ambalo mkuu wa shule hiyo alionekana katika video akiwachapa viboko wanafunzi huku akiwakanyaga miguu.

Sheria ya Elimu sura ya 353 inampa mamlaka Waziri wa Elimu kutunga kanuni za masuala mbalimbali zitakazokidhi utekelezaji wa sheria ambazo zinatoa mwongozo ni wakati gani adhabu ya viboko inaweza kutolewa na kwa kiwango gani.

Kadhalika, kanuni ya 3 (1) ya sheria hiyo inasema adhabu ya viboko itatolewa iwapo patatokea utovu mkubwa wa nidhamu au kosa kubwa litakalofanywa ndani au nje ya shule ambalo litaishushia shule heshima huku kanuni ndogo ya (2) inasema itolewa kwa kuzingatia umri, jinsia na afya ya mwanafunzi na isizidi viboko vinne kwa tukio lolote.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

MOTO KUTETEA WAFANYAKAZI NYUMBANI...

# Laundwa shirika linalo piga hodi 'nyumba kwa nyumba' kudai haki na ulinzi wao kisheria

MIONGONI mwa waajiri ambao wengi ni kinamama kwao hausi geli' ni wa kutumikishwa muda wote. Ndiye mlezi, mpishi, mtunza mifugo na bustani anayelala saa sita na kuamka saa 10 alfajiri.

Hata asipokula, kulipwa kiduchu, kunyimwa mshahara akivunja sahani yote yakiambatana na unyanyasaji mwingi kwa binti huyo, anayechukuliwa kama punda.

Inavyoelekea 'mahausigeli', waajiri na jamii wana elimu duni kuhusu sheria zinazomlinda mfanyakazi huyo wa ndani.

Hayo, yanajidhihirisha kutokana na visa vinavyoripotiwa kuhusu ukatili dhidi yao hasa mijini na kwenye majiji.

Mtumishi wa ndani Beatrice Johnson (27), anazungumza na Nipashe, mwishoni mwa wiki, akisema changamoto alizopitia amezigeuza kuwa fursa.

Pamoja wenzake takribani 30, wanaunda kikundi, ili kuelimisha wafanyakazi wa kazi za ndani na kuwapa mwanga mpya wa kijikomboa.

"Kuna majina mengi wanatuita 'beki tatu' na mengine ya kukebehi ambayo yanaathiri saikolojia ya wafanyakazi wa kazi za ndani. Ukifika dukani kununua kitu unaulizwa wewe ni 'hausigeli', utajibu hapana au utasema naishi na dada yangu.

"Ukianza kuondoka utasikia wakiambiana huyo si mfanyakazi au beki tatu wa fulani, kwa kweli hayo yaliniumiza sana. Kwanza wanaofanya kazi hii wanaishi na watu ambao hawawajui, wanakuwa hawana ujasiri," anasema Beatrice.

"Nimefanya kazi za ndani takribani miaka 10, minane nimekuwa Morogoro baadaye nikaondoka. Kuna unyanyapaa, lakini leo tumewezeshwa kujua haki za kazi."

Anasema walipopata mradi wakabadili kikundi na sasa wameanzisha shirika na ndiye Mkurugenzi wa Shirika la Light for Domestic Workers, lililopo mkoani Morogoro.

Anaeleza namna walivyonufaika na ruzuku kutoka Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFTT) kwa mwaka 2021 na 2022 na kufanikisha kutoa elimu nyumba kwa nyumba kupitia shirika hilo, linalojumuisha wafanyakazi au waliokuwa watumishi wa kazi za ndani.



Beatrice Johnson; Mkurugenzi wa asasi ya Right for Domestics Workers. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

"Tunaelimisha kuepukana na ukatili kijinsia, afya ya uzazi na kuepuka mimba. Kwa sababu kuna matukio mengi baba mwenye nyumba au vijana wao wanawapa mimba wasichana wa kazi. Mabinti kwa kuwa ni wadogo tena wasio na uelewa wanarubuniwa," anasema Beatrice.

Anaongeza kuwa kikundi chao kilichobadilika kuwa Shirika la Mwanga kwa Wafanyakazi wa Nyumbani,

kilianzishwa 2019 na kusajiliwa 2021.

Anasema elimu waliyoitoa imewafikia wasichana wa kazi ambao wengi wao wamemaliza darasa la saba, la nne au hawajasoma.

"Asilimia 90 ya tuliowafikia ni wasichana wadogo. Unaweza ukatembelea nyumba 10, moja ndiyo ina mfanyakazi wa kiume. Kabla ya WFT-T tulijichangisha kulipa kodi, nauli kwenda sehemu kutoa elimu au unaambiwa kuna mgogoro sehemu kuhusu mfanyakazi, ila sasa ruzuku kwa kipindi hicho imewezesha kufikia kata takribani 10, Morogoro mjini.

Anakumbusha kuwa wanalindwa na sheria za kazi, kadhalika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, inamlinda mfanyakazi wa kazi za nyumbani mwenye kuanzia miaka 14.

Anaelekeza afanye kazi zipi ambazo hazimwathiri afya na ndoto yake maishani. Kama anasoma inawezekana akaendelea na masomo akiwa kazini, kama ni muda wa kucheza atacheze sababu bado ni mtoto.

"Mwajiri unatakiwa umwangalie kama mtoto kwa sababu hajafikisha miaka 18 inayotambua kisheria kuwa ni mtu mzima," anasema Beatrice.

Kwa mwaka jana ruzuku hiyo imewafikisha kwa wafanyakazi za ndani 250 na kati yao 150 wamepewa elimu ya mafunzo kwenye semina au kwa kuwafuata ana kwa ana nyumbani.

Aidha, anasema pia, ruzuku imewawezesha kuwafikia waajiri 72 na kuwapa mikataba ili wawapatie wafanyakazi wao na kuwaelimisha kuhusu faida ya maandishi kimkataba na kuwashairi kuishi nao kama familia zao.

"Kuna wakati hata namna ya kumfikia mfanyakazi huyu ni changamoto. Mwajiri anaona kama mnakwenda kumfungua macho, lakini kupitia uongozi wa mtaa wanatambulishwa. Wengine tunawapigia simu kuwakumbusha kuhudhuria semina, sababu mwingine hajui kusoma wala hawezi kujua ujumbe."

"Kwa ujumla changamoto zipo lakini hatukati tamaa, tunakwenda hadi nyumbani, kuwaelimisha ili wajitambue, na si kuwabadili tabia na kutofanya majukumu kikamilifi," anaeleza Beatrice.

Anabainisha kwamba mfanyakazi wa kazi za ndani, analindwa haki zote, akisema changamoto iliyopo ni kwa waajiri wengi kumpangia majukumu yanayomzidi umri.

Kuhusu mikataba na mishahara kwa wafanyakazi hao, Beatrice anaeleza kwamba ni changamoto, kwa kuwa wengi waliowafikia hawana mikataba huku mishahara yao, akilipwa mzazi, mlezi au dalali.

"Tunashawishi kuwe na mikataba ya ajira kwa sababu akishaingia mkataba utamlinda, tunafuatilia kwamba atamlipa lini, makubaliano hayo tunafuatilia. Na je, atamlipa kwanza kisha atume kwao, lakini wakati mwingine unakuta mzazi anawasiliana na mwajiri kuchukua mshahara," Beatrice anafafanua.

"Kwa kuwa mtoto bado ni mdogo mkataba huo una sehemu ya shahidi ya kiongozi wa mtaa, Mtendaji au Mwenyekiti, agonge muhiri inakuwa salama kwao. Hata kama hajui kusoma utatafsiriwa.

**MALIPO MAPYA**

Kuhusu mshahara, Beatrice anasema waajiri wengi hawajafahamu viwango vipya vilivyotolewa Januari mwaka huu, kulingana na Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini.

"Sheria inasema kiwango cha mshahara wa mtumishi aliyeishi na mwajiri ni Sh. 60,000, awali ilikuwa 40,000. Kwa yule anayekwenda kwa mwajiri na kurudi ni Shilingi 20,000 awali ilikuwa 80,000. Kuanzia Januari 2023 utekelezaji umeanza, ila wengi hawana taarifa, tunawaelimisha," anasema.

Kwenye likizo, pia wanahaki hiyo wafanyakazi hao kama ilivyo kazi nyingine, ikiwamo kupatiwa huduma muhimu za kiafya, chakula, makazi hususan kwa wanaoishi na mwajiri.

"Anapokuja mfanyakazi nyumbani kwako hujui ameshakumbana na changamoto ngapi, unakuta ameshafanya kazi zaidi ya nyumba 10 ila ukimhoji hawezi kusema kweli, atasema hii ni nyumba ya pili, anategemea akija kwako apate kitu fulani, akikosa ndio ukatili unaanza," anaeleza Beatrice.

Kutokana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto au wanafamilia majumbani, anasema itungwe sheria ndogo inayowataka wafanyakazi hao kutambulika na viongozi wa mtaa, inapotokea changamoto, ijulikane pa kuanzia.

"Unakuta msichana amefika jana. Leo anaachiwa nyumba nzima. Lakini kuna changamoto ya madalali wa kuwaleta wasichana hao. Wanawafanya kuwa vitega uchumi. Leo kakaa kwako siku 30, dalali anapiga simu kafiwa, anamrudisha kwao Mwanza, kumbe anamtoa mkoa huo huo anapeleka mtaa mwingine."

Anasema kuna rushwa ya ngono, dalali anamrubuni msichana kuwa atampa kazi, kwa hiyo kwa shida anakubali na kushauri wapigwe marufuku kwa kudhalilisha utu.



## Uharibifu mazingira watishia uendelevu miradi ya maji

Na Renatha Msungu, MPWAPWA

UHARIBIFU wa mazingira katika vyanzo vya maji na mabwawa unatishia uendelevu na uwekezaji mkubwa wa serikali katika miradi mingi ya maji nchini, imeelezwa.

Meneja wa Wakala wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mpwapwa, Mhandisi Cyprian Warioba, alieleza hayo juzi katika kikao cha wadau wa maji kilichofanyika wilayani hapo kwa ajili ya kuangalia utekelezaji na utoaji wa huduma za majisafi na salama mjini Mpwapwa.

Warioba alisema katika mwaka wa fedha 2023/2024 serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imepanga kutekeleza miradi ya maji 15 katika maeneo mbalimbali itakayogharimu Sh. bilioni 2.6.

Aidha, alisema idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi na salama hadi Januari 2023 ni 248,727 sawa na asilimia 65.05, ya makadirio ya watu wapatao 320,891.

Hata hivyo alisema kuwa vijiji 48 kati ya 113 vya Wilaya ya Mpwapwa havina huduma ya majisafi na salama na kulazimika kutumia maji ya korongoni au vyanzo vya asili pamoja na kuwa serikali inatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mbalimbali.

Kadhalika, alisema katika mwaka 2022/2023 serikali ilitekeleza miradi saba ya maji katika vijiji vya Mtera, Pwaga, Maswala, Munguwi na Itende.

Vijiji vingine, ni Lupeta, Makutupa mradi wenye vijiji viwili Igoji, Chinyika, Mlunduzi, Kisokwe, Idilo na mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji Kijiji cha Kibakwe, ambapo miradi iligharimu Sh. bilioni 9.2.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Sophia Kizigo, alisema ili kuondokana na tatizo la uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji, RUWASA wanapaswa kuwaajili mgambo watakaopatiwa mafunzo maalum kwa ajili ya kulinda vyanzo hivyo.

Alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika miradi ya maji lazima ulindwe na kuwekewa mkakati wa kudumu ambapo kupitia kikao hicho wadau walikubaliana kuwa na kampeni ya kupanda miti na kulinda vyanzo vya maji ikiwamo kampeni ya kila nyumba kuwa na choo salama.

Mmoja wa wadau wa Shirika la Water for People Tanzania, Rehema Turkai, alisema wako tayari kuunga mkono jitihada za serikali katika afua mbalimbali zinazolenga kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama na usafi wa mazingira.

# Dk. Msonde ataka ubunifu, ushirikishwaji wananchi

Na Paul Mabeja, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde, amewataka watumishi wa umma kuwa wabunifu na kuwashirikisha wananchi kutatua kero zinazowakabili kwa kutumia rasilimali walizonazo.

Alibainisha hayo juzi jijini hapo, alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili ya fursa na vikwazo kwa maendeleo na ugatuzi wa madaraka kwa makatibu tawala, wakurugenzi wa halmashauri na maofisa mipango.

Alisema watumishi wa umma wanapaswa kuwa sehemu ya kusaidia jamii kukabiliana na kero zilizoko kupitia rasilimali zilizoko kwenye maeneo husika.

"Kiongozi legelege hata maendeleo yatakuwa legelege hivyo watumishi wenzangu wa umma tunapaswa kutumia nafasi zetu kuwa wabunifu katika kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wananchi haiwezekani leo hata matundu ya choo watu bado wanasubiri fedha kutoka serikali kuu," alisema Dk. Msonde.

Aidha, alisema wananchi pia wanapaswa kuwa wazalendo katika kuhakikisha waisaidia serikali kujiletea maendeleo kupitia fursa zilizoko bila kusubiri kufanyiwa na serikali.

"Kuna maeneo tulitembelea ujenzi wa madarasa kuna sehemu serikali ilitoa Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa darasa lakini ulikwama tukabaini kuwa maeneo ambayo wamefanikiwa ni kwasababu wananchi walishirikishwa, hivyo viongozi wa umma tunapaswa kuwashirikisha wananchi katika miradi ya maendeleo ili iwe endelevu na yenye tija kwa jamii,"alisema.

Kadhalika alisema kama serikali itakuwa na utaratibu wa kushirikisha wananchi katika miradi kuanzia ngazi ya msingi kwa kutumia mfumo wa ugatuzi wa madaraka ambao utasaidia miradi kuwa na tija kwasababu wao ndiyo watakuwa waibuaji.

"Miradi mingi ya umma inaweza isiwe na tija na kusababishia serikali hasara kutokana na kutoshirikishwa kwa wananchi na kuanzishwa kwa mradi ambao siyo kipaumbele kwa wananchi wa eneo husika hivyo ni busara sasa wananchi kushirikishwa kuibua miradi yao wenyewe ili kujiletea maendeleo," alisema.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri Tanzania (TOA), Jacob Mtalitinya, alisema mafunzo hayo yameratibiwa na umoja huo kwa kuwezesha na Shirika na Maendeleo Japan (JICA) Tanzania.

Mtalitinya alisema lengo la umoja huo ni kubadilishana uzoefu na kuboresha utendaji kazi ngazi ya serikali za mitaa.

Hata hivyo, alisema ipo haja ya kuzijengea uwezo mamlaka za serikali za mitaa nchini ile ziwe na uwezo wa kujiendesha na kutumia fursa na vikwazo kwa maendeleo ili kuwaletea maendeleo wananchi wake.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), Mhandisi David Pallangyo, akizungumza na waandishi wa habari Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma jana, alipoelezea mafanikio na majukumu ya mamlaka hiyo, wamepokea Sh. bilioni 220 kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanisa AGGCI laiangukia serikali kupata usajili wa kudumu

Na Paul Mabeja, DODOMA

KANISA la Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI), limeomba serikali kuwapatia usajili wa kudumu ili kushiriki katika jitihada za kuilinda na kudumisha amani ambazo zimekuwa zikifanywa na serikali.

Katibu Mkuu wa AGGCI, Dk. Robert Ngai, alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa maombi hayo kwa Msajili wa Serikali wakati wa mkutano mkuu wa kanisa hilo jijini hapo.

Alisema kutokana na kanisa hilo kuwa na usajili wa awali wanashindwa kutekeleza baadhi ya mambo ambayo yangesaidia kuendeleza ulinzi wa amani iliyoko nchini.

"Hivi sasa kanisa letu linausajili wa awali hivyo kwa mujibu wa sheria kuna baadhi ya vitu hatutakiwi kuvifanya ikiwamo kufungua matawi lakini kufanya mikutano ya hadhara, hivyo basi tunaiomba serikali yetu itusaidie kupata usajili wa kudumu ili tushiriki katika kuendeleza amani iliyoko nchini mwetu.

"Unapohubiri unapata waumini wapya lakini sasa hatuna pakuwapeleka, kwa kuwa hatuwezi kwa sasa kufungua matawi mapya hadi hapo tutakapopatiwa usajili wa kudumu," alisema.

Aidha, alisema wanaishukuru serikali ambavyo imekuwa ikishiriki kulinda na amani ya nchi na kuleta suluhu na maridhiano miongoni mwa Watanzania.

Akizungumzia kuhusu kuongezeka kwa vitendo vya ukali nchini alisema viongozi wa dini kila mmoja anaowajibu wa kuhakikisha kuwa anahubiri neno la Mungu kwa ufasaha bila kuweka maslahi binafsi.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa serikali pamoja na Watanzania kwa ujumla kumrudia Mungu ili kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa kadri ambavyo amepewa nafasi bila kuweka maslahi yake mbele.

Vile vile, aliwataka waumini wa kanisa hilo kuwa watulivu na wavumilivu katika kipindi chote ambacho watakuwa wanasubiri mchakato wa kupatiwa usajili wa kudumu kukamilika.

Kanisa la Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI), limezaliwa kutokana na mgogoro wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT) ambapo baadhi ya viongozi na waumini waliondoka na kuanzisha kanisa jipya.





# Mkandarasi Uwanja wa Ndege Songwe apewa muda

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Mbeya, imemwagiza mkandarasi anayejenga jengo la abiria Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) kukamilisha mradi huo kabla ya Aprili mwaka 2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Mkoa, Juma Homera alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki walipokagua ujenzi wa jengo hilo ambao kwa muda mrefu umesuasua.

Alisema kwa kuwa wamewavumilia kwa muda mrefu sasa wametoa ukomo wa muda kuwa ifikapo Aprili 2024 jengo hilo liwe limekamilika kabla hatua za kinidhamu hazijachukuliwa.

Alisema mradi huo unagharimu zaidi Sh. bilioni 33 na kumtaka mkandarasi mshauri wa jengo hilo kukamilisha kazi zilizobaki ili jengo lianze kutumika.

"Jengo hili ujenzi wake ulianza muda mrefu lakini unasuasua serikali inatoa fedha lakini hatuoni likikamilika mpaka sasa, tunaagiza mpaka kufikia Februari mwaka 2024 liwe limekamilika vinginevyo hatua zitachukuliwa," alisema Homera.

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matari Masige, alisema tayari ujenzi umefikia asilimia 95 ya matengenezo licha ya kinachokwamisha ni vifaa kuchelewa.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliwashauri wakulima wa mazao kutumia usafiri wa anga kusafirisha mazao yao na kujiingizia kipato kwa haraka kuliko ilivyo sasa ambapo hutumia zaidi usafiri wa barabara.

Mwakibete alitoa kauli hiyo alipotembelea uwanja huo wa ndege kwa lengo la kujionea ukarabati wa jengo la abiria.

Alisema kuna fursa nyingi kwenye usafirishaji wa anga ambazo mkulima na mfanyabiashara atazipata ikiwamo kuwahisha bidhaa sokoni.

"Mkoa wetu unazalisha mazao mengi ya chakula na biashara na tunatumia zaidi usafiri wa barabara kuliko anga sijui kwa nini mwitikio ni mdogo nawahamasisha kutumia usafiri huu mtapata faida lukuki ikiwamo kuwahisha mazao yenu sokoni lakini inaokoa muda," alisema Mwakibete.



Kamishna wa Jeshi la Polisi nchini, Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Suzan Kaganda, akimkabidhi cheti mwanafunzi bora wa masomo ya sayansi, Myla Matondane, kwenye mafahali ya wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Wasichana ya Barbro Johansson jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni mwanzilishi wa Joha Trust, Prof. Anna Tibaijuka. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Afikishwa kortini kuvamia shamba lenye mgogoro wa mirathi

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

MKAZI wa Kijiji cha Kyimo wilayani Rungwe mkoani Mbeya, Innocent Mwakamele, amefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo ya Tukuyu, akituhumiwa kuvamia shamba lenye mgogoro na kukata miti ya mbao.

Msimamizi wa shamba hilo, Alune Mwandemele ndiye alifungua shauri hilo mahakamani na kumtaka kujibu tuhuma zinazomkabili ikiwamo kuidharau mahakama baada ya kumpa barua ya wito mara kadhaa.

Alune alisema mahakama ilitoa amri ya kutofanyika shughuli zozote mpaka shauri la mirathi litakapofanyiwa maamuzi lakini Innocent alikaidi na kukata miti hiyo.

"Shauri la mirathi namba 54/2020 lilifunguliwa Mahakama ya Mwanzo Mjini Tukuyu baada ya Osiah Mwandemele kufariki dunia, familia yake ilifanya kikao na kumchagua Alune Mwandemele kusimamia mgawanyo wa mali za marehemu ambazo ni nyumba na mashamba," alieleza Alune.

Baada ya kufikishwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mji wa Tukuyu, Ally Mgomba, mtuhumiwa Innocent alikiri kutenda kosa na kudai alitumwa na Fredy Mwandemele ambaye ni mmoja wa wanafamilia ambaye alikana kuhusika na suala hilo.

Alune aliiomba mahakama kuwa apatiwe Sh. 200,000 kama gharama aliyoitumia kumtafuta mtuhumiwa Innocent ambaye alitoroka baada ya kukata miti ambapo alikubali kulipa fedha hizo na kuzilipa mbele ya mahakama na kusaini karatasi ya makabidhiano.

Hata hivyo uamuzi wa shauri hilo, utatolewa Machi 27, mwaka 2023, ambapo familia ya Mwandemele itatoa maelezo ya mirathi yao licha ya kuwa mpaka sasa kuna mgogoro baina yao kuhusu wasimamizi waliopo baadhi wakitaka waondolewe.

# 'Ujenzi usiofuata ramani una madhara kiafya'

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

IMEELEZWA kuwa ujenzi holela unasababisha madhara ya kiafya kwa binadamu kutokana na kukosa mzunguko wa hewa safi unaosababishwa na mpangilio mbovu wa majengo.

Hayo yamebainishwa juzi na Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu wa Wakadiriaji wa Ujenzi, Edwin Nnunduma, wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa ubunifu na ukadiriaji wa majenzi jijini Mbeya.

Nnunduma alisema watu wengi hudhani kupanga miji sio jambo la muhimu hivyo hujenga mahali popote bila kuzingatia kanuni za kitaalamu katika ujenzi hali ambayo imekuwa ikisababisha madhara ya kiafya yakiwamo magonjwa yanatokana na kuvuta hewa chafu.

"Kuna jinsi ya kujenga nyumba kwa kuzingatia mzunguko wa hewa mfano ukijenga kiholela huwezi kujua madirisha yako yakae vipi, choo kiwe wapi au nyumba inaweza kutazama sehemu ambazo jua halifiki au uko karibu na maji machafu yanatiririka hapo, watu wengi wanaona na sawa tu lakini madhara yake ni makubwa," alisema Nnunduma.

Alisema hali hiyo inasababishwa na wananchi wengi kutowatumia wataalamu wa ubunifu na ukadiriaji wa ujenzi badala yake wanawatumia watu wasio na utaalamu wa kutosha ambao hawana uwezo wa kuwashauri kuhusu kanuni bora za ujenzi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alisema wananchi wengi wanashindwa kuwatumia wataalamu hao katika shughuli zao za ujenzi kutokana na kuhofia gharama kubwa na kuwataka wataalamu hao kuwa na gharama rafiki zinazoendana na kipato cha wananchi.

Aidha, alisema wananchi wengi hawana elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa kuwatumia wataalamu hao katika shughuli zao za ujenzi hivyo wanapaswa kuwa na mikakati ya jinsi ya kuwafikia wananchi ili kuwapa elimu hiyo.

"Sasa hivi katika kila wilaya na halmashauri zetu kuna majengo makubwa yanajengwa lakini wanashindwa kuwatumia kwa sababu muda mwingi nyie wataalamu mko mjini hamjaenda huko na hii elimu hawana hivyo kama elimu yenu haitumiki basi mnapoteza maana," alisema Mayeka.





## Nyumba zilizoathiriwa na mradi wa gesi zaanza kuhakikiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesema kuwa imeshirikiana na wataalamu wa majengo kutoka Chuo Kikuu cha Taifa SUZA, kuzikagua, kuzihakiki pamoja na kuzitathmini nyumba zote zilizoharibiwa kutokana na mchakato wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtambwe, Habib Ali Mohamed.

Mwakilishi huyo alitaka kujua, zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kisiwani Pemba, kuna wananchi ambao nyumba zao ziliathirika katika mchakato huo.

Alisema ulipaji wa fidia kwa nyumba hizo ulifanyika kwa mujibu wa kiwango cha athari kilichojitokeza ambapo hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

"Kwa mantiki hiyo, serikali inaamini kwamba viwango hivyo vilivyolipwa vinaendana kwa mujibu wa athari husika ambapo hadi sasa kazi ya ulipaji wa fidia inaendelea,"alisema.

Alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mafuta Zanzibar (ZPRA) inaendelea na hatua za kuyafanyia kazi malalamiko yanayowasilishwa kwa kuyawasilisha kwa mkandarasi ili kuondokana na matatizo hayo.

**Mwakilishi huyo alitaka kujua, zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kisiwani Pemba, kuna wananchi ambao nyumba zao ziliathirika katika mchakato huo.**

# SMZ yachukua hatua madhubuti kuwainua wanawake kiuongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amesema kwa kipindi kirefu wanawake wameachwa nyuma katika uongozi, hivyo juhudi mbalimbali zimechukuliwa kimataifa na kikanda ili kuwainua.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya tuzo za uandishi wa habari za takwimu za wanawake na uongozi zilizoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi za Zanzibar.

Alisema miongoni mwa juhudi hizo ni kupitishwa kwa mkataba wa kuondosha aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake CEDAW ya mwaka 1979, itifaki ya Maputo ya mwaka 2003 ambapo ni moja ya juhudi za Afrika kuwainua wanawake.

Alisema pia mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2008 unaosisitiza ushiriki sawa wa wanawake kufikia asilimia 50/50 kwenye nyanja za maamuzi serikalini na taasisi binafsi.

"Lazima tukiri kuwa bado usawa katika nafasi za uongozi umekuwa na tatizo na serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuimarisha masuala ya wanawake na uongozi na kuongozwa na mikataba ya kitaifa na kikanda na azimio la Beijing hii ni kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanapata nafasi sawa ya kushiriki katika ngazi zote za uongozi,"alisema.

Alisema suala la mwanamke na uongozi ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii na ndiyo maana katika Dira ya Zanzibar ya mwaka 2050 inatambua ulazima huo wa kujenga usawa katika jamii.

Alisema wanawake wakiwa katika vyombo vya maamuzi watapunguza umaskini wao na kuzungumzia matatizo yanayowakabili na hisia zaidi na kurahisisha kufanyiwa kazi.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdallah Said, alisema kuwa lazima kuwaandaa wanawake kujiamini tokea wakiwa shuleni ili kuchukua nafasi za uongozi.

"Wizara ya Elimu itashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha tunajenga uwezo wa vijana wetu wakiwa katika ngazi ya shule kujiamini na baadaye kuchukua nfasi mbalimbali za uongozi,"alisema.

Alisema wizara inaprogramu ya kuanzisha kambi ya sayansi, hesabu na ubunifu ili kuwaongezea vijana wa kike kujiamini na kuwajengea stadi za maisha ili kuwa viongozi wakubwa wa nchi.Alisema kazi inayofanywa na waandishi wa habari wanawake ni nzuri zaidi katika kuhamasisha masuala ya wanawake katika uongozi.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema waandishi wa habari ni nyenzo kubwa ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii, hivyo kuwekeza kwenye waandishi wa habari kutafikisha katika usawa wa kijinsia katika vyombo vya maamuzi.

Alisema bado njia ya kufika katika usawa wa kijinsia haipo sawa bali imesheheni vikwazo vingi licha ya wanawake ndio wapiga kura wengi lakini wanakumbana na vikwazo vingi wanapotaka kugombea nafasi za uongozi ikiwamo kutishwa, udhalilishaji katika mitandao ya kijamii, rushwa, uhaba wa fedha, woga wa kutohimili mapigo ya kisiasa kutokana na majungu na uelewa mdogo wa haki zao.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa viongozi wanawake ni wachapakazi wakubwa, waaminifu na wanaopenda kushirikishwa hivyo waandishi wa habari wanafasi kubwa ya kubadilisha mawazo hasi na kubadilisha hali ya ushiriki mdogo wa wanawake katika uongozi.




Baadhi ya mawaziri wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakishi kutoka kushoto ni Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, Waziri wa Ardhi na Makazi, Rahma Kassim Ali na Waziri wa Maendeleo ya Ustawi ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi barabara Wete - Chakechake kukamilika mwakani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema mchakato wa kulipa fidia kwa wananchi walioathirika na mali zao kupisha ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake Chake unaendelea vizuri ambapo ujenzi umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kumalizika Julai mwakani.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif Yussuf, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtambwe, Habib Ali Mohamed aliyetaka kufahamu kwa nini ujenzi wa barabara hiyo haukamiliki kwa wakati.

Akijibu swali hilo, alisema mchakato wa fidia umechelewa baada ya kubainika kuwapo kwa watu walioingizwa kinyume na sheria kwa kufanya udanganyifu ambapo serikali imeanza kuchukua hatua za kinidhamu.

Alisema serikali tayari imeanza kutoa maagizo kwa vyombo vya sheria ikiwamo Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kuwachunguza watu ikiwamo watendaji waliofanya udanganyifu huo.

"Mheshimiwa ni kweli ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete umechelewa kidogo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuchelewa kulipa fidia kwa watu waliohusika na mali zao kuathirika na kupisha ujenzi wa barabara ambapo baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu wametumia mwanya kuwaingiza watu wasiohusika ambapo tumeanza kufanya uchunguzi," alisema.

Akifafanua zaidi alisema Wizara ya Ujenzi tayari imewataka makandarasi wote waliopewa kazi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara kuhakikisha wanakamilisha kazi hizo kwa wakati.

Aidha, alisema Wizara ya Ujenzi haitokubali kuona makandarasi wanapewa stahiki zao kwa wakati lakini wanashindwa kukamilisha kazi kwa wakati husika na kukabidhi serikalini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA.23 YA MWAKA 2023.**
**MAOMBI YA NARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HASSAN SAAD KITETE**
**MADUA YUSUPH IBRAHIM......1 MWOMBAJI**
**HENRY HASSAN SULEIMMAN...2 MWOMBAJI**

### TAARIFA YA KAWAIDA
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kuja na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe ya 13 mwezi wa Aprili, 2023.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 20 mwezi wa februari ,2023

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. …./2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JUMA SELE SUSA wa DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NUSURA HUSSEIN MUSSA**

### TANGAZO
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 Mwezi March Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 02 Mwaka 2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA)**
**Mahakama ya Mwanzo ya ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA MJINI**
**MADAI NAMBARI 30 ya 2023**
**Mdai: KHAMIS ABDULRAZAK MOHAMED**
**Mdaiwa: TAMIMA YUSSUF KHAMIS**
**Kwa: TAMIMA YUSSUF KHAMIS**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/ Wameleta madai yake/ yao kwamba **(Eleza hapa habari za madai)**
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA TALAKA NA MATUNZO YA WATOTO.**
Kwa hiyo unahitajiwa/ Mnahitajiwa kuhudhuria mahakama hii siku ya **IJUMAA** Tarehe **10/03/2023 Saa 2:30** asubuhi/ alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/ wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuudhuria / hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa / mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 24/3/2023.

---

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha: MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 19/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**ABDULRAHMAN ALLY MSANGI WA BOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY ABDULRAHMAN MSANGI**

### TANGAZO
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03/ Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 02 mwaka 2023**

---

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 15/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**ASIA RAJABU MATITU WA IRAMBA SINGIDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA JOHA SULTAN MZUZURI**

### TANGAZO
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 / Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 27 mwezi 02 mwaka 2023**

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GLORIA STEVEN BUKUKU** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye Namba **TAE 311741.** Iliyotolewa Dar es salaam **PCO mwaka 2020.** Kwa Yeyote ataekaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIL/RB/ 77347/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**ANTIDIUS EVALIUS RUTAIHWA**, Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **Index no S4327-0054** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIBETA SECONDARI Mwaka 2020.** Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/75439/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LECKSON FEDRICK MABENA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S5105-0032** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **UMAWANJO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI CONTROLL NAMBA: **9910836182842**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSA HUSSEIN MTONGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 509 DLW – TOYOTA ALPHARD.** Chassis namba **ANH100054757.** Engine namba **2AZ1350692.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/77229/2023.**

***OFISI ZA MATANGAZO***
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Matokeo ya uchaguzi yaanza kutangazwa majimbo Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

TUME ya Uchaguzi nchini Nigeria (INEC) imeanza kutangaza matokeo ya majimbo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Jumapili, huku vyama vyote vikilalamikia upungufu na ukiukwaji wa sheria na kanuni za uchaguzi.

Matokeo ya kwanza kutoka jimbo la Ekiki yalionyesha kura nyingi zilikwenda kwa mgombea urais wa chama tawala (APC), Bola Tinubu, ambaye alijikusanyia kura 200,000 dhidi ya Atiku Abubakar wa chama kikuu cha upinzani cha (PDP) aliyepata chini ya nusu ya kura hizo, huku Peter Obi wa Chama cha Labour akipata kura 11,000.

Baada ya kutangaza matokeo hayo ya awali jana, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Mahmoud Yakubu, alisitisha kikao akisema kuwa kura zinaendelea kujumuishwa.

Hata hivyo, vyama vyote vitatu vililalamikia kuwapo kwa ukiukwaji wa sheria na kanuni za uchaguzi katika matukio kadhaa.

Chama cha Labour ambacho mgombea wake wa urais alitazamiwa kuonyesha upinzani mkali kwa wagombea wa vyama viwili vikubwa, kiliikosoa vikali tume hiyo ya uchaguzi kwa kushindwa kuyapandisha matokeo kwenye tovuti yake kama ilivyoahidi kwa ajili ya kuhakikiwa.

Inaelezwa kuwa zaidi ya saa 24 tangu vituo kutakiwa kufungwa, vingi vyao vilikuwa bado havijayapandisha matokeo mtandaoni.

Muungano wa asasi za kiraia nchini humo ulilalamikia makosa na kushindwa kufunguliwa vituo kadhaa kwa wakati.

Tume ya Uchaguzi iliomba radhi kwa makosa hayo kupitia taarifa yake ikisema inafahamu changamoto zilizoko kwenye mfumo wake wa kuangalia matokeo, ambao umekuwa na kasi ndogo sana kutokana na hitilafu za kiufundi.

Vyama vya APC na PDP vililalamika kwamba maofisa wa tume ya uchaguzi walikuwa wakishinikizwa kuharibu matokeo kabla ya kuyawasilisha kunakohusika.

Inaelezwa kuwa wanajeshi waliingilia kati baada ya watu 15 waliojifanya maofisa wa tume ya uchaguzi kuvamia kituo cha kukusanyia matokeo katika kitongoji cha Alimosho, karibu na mji mkubwa wa kibiashara Lagos na kuwashambulia mawakala wa vyama kwa visu na magongo.

Katibu wa Chama cha Labour katika eneo hilo, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba wavamizi hao walimpiga kila mtu waliyemdhania kuwa mwanachama wa chama chake.

Hata hivyo, wanajeshi waliwatia nguvuni watu wote 15 waliohusika na tukio hilo.

Kura za urais na ubunge hukusanywa kwenye kila jimbo kati ya majimbo 36 ya Nigeria kabla ya hesabu zake kupelekwa kwenye kituo kikuu cha majumuisho katika mji mkuu, Abuja.

***DW***



Waokoaji wakiokoa mwili kwenye fukwe karibu na Cutro, kusini mwa Italia baada ya boti lililokuwa limebeba wahamiaji kuzama baharini jana. **PICHA: AP**

## Makumi ya wahamiaji wafariki dunia Italia

**CROTONE, Italia**

TAKRIBANI wahamiaji 59 pamoja na mtoto mchanga wa miezi wamefariki baada ya boti waliokuwamo kuzama, alfajiri ya Jumapili karibu na mji wa Italia wa Crotone, huko Calabria Kusini.

Inaelezwa kuwa boti hiyo ya takriban mita 20 ilisafirisha wahamiaji 250 wenye asili ya Afghanistan, Iran na Pakistan na ilizama kutokana na dhoruba kali, dhidi ya miamba karibu na fukwe ya Steccato di Cutro.

Akitoa tathmini ya ajali hiyo jana Meya wa Crotone, Vincenzo Voce, alibainisha kuwa watu 70 walinusurika katika ajali hiyo wakiwamo 21 ambao wamelazwa hospitalini na kwamba zoezi la kutafuta miili ya watu wengine linaendelea kwa shida kutokana na hali ya hewa, upepo mkali na mawimbi makubwa.

Rais wa eneo hilo, Roberto Occhiuto, alilalamika akisema "Makumi wamekufa maji wakiwamo watoto wengi wametoweka, Calabria iko katika maombolezo ya msiba huu mbaya."

Ilibainishwa kuwa boti hiyo iliondoka kwenye bandari ya Smirna siku nne zilizopita na kwamba ndege ya Frontex iliiona karibu na Crotone jana jioni na kutoa taarifa ya uokoaji wa baharini kutoka Taranto na Crotone lakini hali mbaya ya hewa ilizuia kufikia eneo hilo.

Waziri Mkuu, Giorgia Meloni, alionyesha kutoridhishwa na tabia ya usafirishaji haramu wa binadamu, akisisitiza dhamira ya serikali yake kuzuia uhamiaji haramu.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Matteo Piantedosi, alimuunga mkono kwa kuzungumzia janga kubwa linalodhihirisha kuwa ni muhimu kupambana na mitandao ya wahamiaji haramu.

***RFI***

# Majanga yazikumba jamii za Niger na Cameroon

**DIFFA, Niger**

MAOFISA wa Cameroon na Niger wamesema kwamba mamilioni ya watu kutoka maeneo yaliyoathiriwa na mashambulizi ya wanamgambo wa Boko Haram wanakabiliwa na tishio la hali mbaya ya njaa na mafuriko.

Hayo yalisemwa na magavana kutoka mataifa yote mawili waliotembelea kaskazini mwa Cameroon Ijumaa na walisema mamilioni ya watu wakiwamo waliotoroka ghasia kati ya wakulima, wavuvi, wafugaji na wanaorejea makwao wanahitaji misaada ya chakula pamoja na usaidizi wa makazi.

Maofisa kutoka Halmashauri ya Ziwa Chad, walisema mamilioni ya wakimbizi pamoja na watu waliokoseshwa makazi wanaorejea kwenye miji na vijiji vya Cameroon, Chad, Nigeria na Niger wanahitaji misaada ya dharura ili kuokoa maisha.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN) kundi la kigaidi la Boko Haram kwenye maeneo hayo limeacha zaidi ya watu 36,000 wakiwa wamekufa hasa nchini Nigeria, wakati takriban milioni tatu wakilazimika kutoroka makwao.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo inayojumuisha magavana wanane kutoka majimbo yaliyoathiriwa na Boko Haram, Midjiyawa Bakari, alisema alitembelea majimbo hayo nchini Niger na Cameroon mwishoni mwa wiki, ili kujionea changamoto wanazopitia wale wanaorejea kwenye miji na vijiji vyao.

"Migogoro kadhaa imeripotiwa miongoni mwa watu wanaorejea kwenye maeneo yanayozunguka ziwa Chad takriban watu milioni 40, ziwa hilo limepungua kwa asilimia 60 ndani ya miaka 60 iliyopita, wakazi wa eneo hilo wanategemea ufugaji, uvuvi na ukulima.

"Tumefanya mkutano wa dharura na gavana wa jimbo la Diffa Mohamed Mouddour ili kujionea namna maisha ya mamilioni ya watu yalivyoathiriwa na namna yanavyoweza kuimarishwa, pamoja na kuhakikisha usalama wao dhidi ya mashambulizi kutoka kundi la Boko Haram," alisema.

Bakari ambaye ni gavana wa jimbo la kaskazini mwa Cameroon la Far North, alisema mabadiliko ya hali ya hewa yamesababisha mizozo kati ya wafugaji, wavuvi na wakulima kutokana na uhaba wa maji mizozo inaripotiwa kila wiki.

Ofisi ya UN ya masuala ya kibinadamu (OCHA) inasema mwaka huu mamilioni ya watu walioathiriwa watabaki kwenye hali tete kutokana na kutokuwapo misaada ya kibinadamu ya kutosha.

OCHA inasema dola bilioni 2.53 zinahitajika ili kukabiliana na mzozo wa kibinadamu uliopo katika kusaidia takriban watu milioni 7.4.

***VOA***

# WACHEZAJI SIMBA, YANGA WANG'ARA IHEFU IKIUA

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI waliotoka Klabu za Simba na Yanga, wakijiunga na Ihefu kwenye kipindi cha dirisha dogo, wameendelea kuibeba timu hiyo na kuipandisha hadi nafasi ya nane ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ijumaa iliyopita, kiungo anayeichezea timu hiyo kwa mkopo akitokea Simba, Mnigeria, Nelson Okwa na straika aliyetoka Yanga raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne, kila mmoja alifunga bao lililoiwezesha timu hiyo kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Licha ya kucheza ugenini, uwezo wa wachezaji hao ambao walikosa nafasi kwenye klabu walizotoka, uliwafanya Ihefu kuondoka na ushindi huo.

Alikuwa ni Okwa ambaye alisajiliwa na Simba msimu huu akitokea Rivers United ya Nigeria, akifunga bao dakika ya 40, kabla ya Yacouba ambaye majeraha ya muda mrefu yalimfanya kukaa zaidi ya nusu mwaka bila kucheza, kupachika bao la pili dakika ya 45.

Mchezaji Vicent Akpan, Mnigeria anayeichezea timu hiyo kwa mkopo akitokea Simba, ambayo ilimsajili kutoka Coastal Union naye alicheza kwenye mechi hiyo.

Yacouba, ambaye Yanga ilimsajili kutoka Asante Kotoko ya Ghana, pia alifunga bao Februari 12, wakati Ihefu ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya.

Kwa mechi hizi tu mbili ambazo wameanza kucheza, Yacouba tayari ana mabao mawili kwenye orodha ya wafungaji msimu huu, huku Okwa naye akifungua akaunti yake ya kucheka na nyavu.

Ihefu ambayo iliburuza mkia kwa muda mrefu katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu na baadhi ya mashabiki kuitabiria kuwa huenda ikashuka tena daraja, ipo kwenye nafasi ya nane ya msimamo ikiwa na pointi 30 mkapa sasa.

Imecheza mechi 24, ikishinda tisa, sare tatu na kupoteza 12, ikiwa imebakisha mechi sita tu kukamilisha michezo 30 ya msimu huu wa 2022/23.

**POLE...**




Watoa huduma ya kwanza wakimsaidia mshindi wa kwanza wa mbio za Kilimanjaro Marathon kilomita 42, Sarah Ramadhani, baada ya kumaliza mbio hizo zilizofanyika mjini Moshi, Kilimanjaro juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zimamoto yaitibulia KVZ mbio za ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Zimamoto imetibua mipango ya safari ya kurahisisha mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa KVZ baada ya kuilazimisha sare ya bao 1-1 katika mwendelezo wa ligi hiyo juzi.

KVZ ingefanikiwa kupata alama tatu katika mchezo huo wa juzi wangekuwa na tofauti ya alama moja dhidi ya vinara wa ligi hiyo, KMKM wenye pointi 47.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KVZ, Ali Khalid, alisema hayakuwa matokeo waliyoyatarajia katika mchezo huo ambapo ungezidisha matumaini na malengo ya yao ya kutwaa ubingwa.

Alisema wachezaji walicheza vizuri na kujituma, lakini haikuwa bahati kwao kupata alama tatu na badala yake waligawana pointi.

Hata hivyo, Khalid alisema matokeo hayo hayajawakatisha tamaa katika mbio za ubingwa, hivyo wataendelea kupambana mpaka malengo yao yatimie.

"Tulicheza vizuri na tulijiandaa kupata alama tatu, lakini ilishindikana na matokeo yake tulipata sare, haya hayakuwa matokeo tuliyoyatarajia, hivyo hatuna budi kujipanga kwa michezo ijayo," alisema Khalid.

Aidha, alisema kwa sasa wanajipanga kuelekea mchezo wao wa raundi ya 23 dhidi ya Uhamiaji FC utakaopigwa katika Dimba la Amaan Jumamosi wiki hii.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa KVZ kuendelea kutoa hamasa kwa timu yao ili kiu yao ya ubingwa imalizike msimu huu na kutovunjika moyo kwa matokeo mabaya waliyoyapata.

# Kali: Kila mechi presha Ligi Kuu

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Kali Ongala, amefunguka kuwa kila mchezo wanaocheza umekuwa mgumu na presha ya hali ya juu katika mzunguko huu wa pili lakini wanapambana ili kumaliza katika nafasi nzuri.

Azam FC ipo nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 47 ikicheza michezo 24 huku ikiwa imebakiza michezo sita kukamilisha mzunguko wa Ligi katika msimu huu wa 2022/23.

Akizungumza na Nipashe jana, Kali alisema mechi za mwisho zina ugumu na presha kubwa, hivyo wanahitaji kupambana ili kuweza kumaliza katika nafasi za juu.

"Tunachotakiwa hivi sasa ni kujiimarisha ili tuwe bora kwa sababu kila mechi inayochezwa inakuwa na presha ya aina yake, ukiangalia huko nyuma tulitoka sare dhidi ya Simba, hivyo tunahitaji kujipanga ili kufanya vizuri katika michezo iliyobaki.

"Muhimu kwetu tunachokiangalia ni alama tatu katika kila mchezo, mfano kwenye mechi ukiongoza goli moja lazima wapinzani wenu na wao watapambana ili warudishe, hivyo tunahitaji kuwa makini, nawasifu wachezaji wangu kwa kupambana," alisema Kali.

Aidha, aliongeza kuwa, anafurahishwa na kiwango cha Prince Dube kutokana na kupambana na kuweza kufunga mbele ya waliomzidi.

"Ninafuraha kuwa na mchezaji aina ya Prince Dube, dogo anajua kupambana kila mechi na kuweza kupata nafasi mbele ya washambuliaji wengine, tunaendelea kumpa mechi tofauti ili aweze kuwa vizuri zaidi," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**LEAO AWANIWA PSG**
KLABU ya Paris St-Germain itakabiliana na ushindani kutoka kwa Liverpool kuwania saini ya mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, huku klabu hiyo ya Merseyside ikiwa tayari kumjumuisha winga wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 26, katika mkataba wa kubadilishana mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

**XHAKA KUFUNGWA ARSENAL**
ARSENAL inafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Uswisi, Granit Xhaka, mwenye umri wa miaka 30, kuhusu kuongezwa mkataba mpya wa miaka miwili. ***(CaughtOffside)***

**SAVIC AWANIWA ARSENAL**
KLABU za Arsenal, Newcastle United na West Ham, zimetoa ofa ya karibu euro milioni 40 kumnunua kiungo wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, 27. ***(Calciomercato)***

**TIERNEY AWINDWA NEWCASTLE**
NEWCASTLE United inapanga kumnunua beki wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 25 wakati wa msimu wa joto. ***(Mirror)***

**RAYA AMULIKA KOMBE**
GOLIKIPA wa Brentford na Hispania, David Raya, amesema anataka "kupigania kushinda taji" huku klabu kadhaa za Ligi Kuu Engand zikiwania saini yake. ***(Athletic)***

**PSG KURUHUSU NYOTA**
KLABU ya Paris St-Germain iko tayari kuruhusu baadhi ya wachezaji nyota wao kuondoka msimu huu wa majira ya joto kwani wanataka kupunguza bili yao ya mishahara kwa asilimia 30. ***(Times)***

**SHEIKH KUONGEZA OFA**
SHEIKH Jassim bin Hamad Al Thani na Kundi la Ineos la Jim Ratcliffe wangehitaji kuongeza ofa zao za awali ili kuishawishi familia ya Glazer kuiuza Manchester United. ***(Telegraph)***

**OMOBAMIDELE AFUATILIWA**
KLABU ya Nottingham Forest inamfuatilia mlinzi wa Norwich na Jamhuri ya Ireland, Andrew Omobamidele mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

**GYOKERES NA EVERTON**
EVERTON na Bournemouth zinamfuatilia mshambuliaji wa Coventry City, Viktor Gyokeres, 24. ***(Football Insider)***




# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH SASA ANUKIA KUTIMKA LIVERPOOL

**Kisa Ligi ya Mabingwa Ulaya, PSG yatajwa kuwa tayari kuweka mzigo mezani huku...**

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah yuko tayari kuondoka Liverpool ikiwa watashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao huku 'Wekundu' hao nao wakiwa tayari kumuuza, kwa mujibu wa Fichajes.

Uvumi kuhusu mustakabali wa Salah hapo Liverpool umezuka upya huku klabu hiyo ikiwa inakabiliwa na changamoto nyingi.

Liverpool wanaonekana kuwa na nafasi ndogo ya kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwani kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora walifungwa mabao 5-2 na Real Madrid nyumbani.

Pia kwenye msimamo wa Ligi Kuu England wanashika nafasi ya saba na wako pointi tisa nje ya nafasi nne za juu za kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kwa mujibu wa Football Insider, Klabu ya Paris Saint-Germain inamtaka raia huyo wa Misri, ambaye ana mkataba na Liverpool hadi katikati ya mwaka 2025 na wataweka dau la euro milioni 80 kwa ajili ya huduma yake.

Liverpool wanaweza kuwa tayari kutoa ofa kwa Salah kutokana na wingi wa chaguo lao la mshambuliaji huku kocha Jurgen Klopp akipania kukirekebisha kikosi chake.

Kwa sasa Liverpool inapambana kuwania saini ya Jude Bellingham wa Borussia Dortmund, ambaye anatarajiwa kugharimu zaidi ya euro milioni 110.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,083,8

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 28 FEBRUARI NA 01 MACHI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13


| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/02/23 | 22:45 | Preston vs Coventry | 2.46 | 3.19 | 2.70 |
| 02. 28/02/23 | 22:45 | Barrow vs Salford City | 2.46 | 3.15 | 2.90 |
| 03. 28/02/23 | 22:45 | Gillingham vs Bradford City | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 28/02/23 | 23:00 | Luton Town vs Millwall | 2.27 | 3.15 | 3.00 |
| 05. 01/03/23 | 19:00 | Slovacko vs Bohemians | 2.35 | 3.37 | 2.64 |
| 06. 01/03/23 | 19:00 | Farco FC vs Arab Contractors | 3.63 | 2.78 | 2.27 |
| 07. 01/03/23 | 20:00 | NK Osijek vs Hajduk Split | 2.69 | 3.11 | 2.46 |
| 08. 01/03/23 | 22:15 | FC Sion vs FC Lugano | 2.51 | 3.31 | 2.51 |
| 09. 01/03/237 | 22:15 | St. Gallen vs FC Basel | 2.26 | 3.48 | 2.70 |
| 10. 01/03/23 | 23:00 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.98 | 2.98 | 2.48 |
| 11. 01/03/23 | 20:00 | Aalborg vs Viborg FF | 2.80 | 3.27 | 2.29 |
| 12. 01/03/23 | 22:45 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.45 | 3.30 | 2.67 |
| 13. 01/03/23 | 23:00 | Real Madrid vs Barcelona | 2.51 | 3.34 | 2.65 |

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI AKASIRISHWA NA KIPIGO CHA BARCELONA



**BARCELONA, Hispania**

XAVI Hernandez alikasirika kwa "uchezaji mbaya zaidi wa msimu huu" baada ya Barcelona kupoteza 1-0 dhidi ya Almeria na kukosa nafasi ya kusonga mbele kwa pointi 10 zaidi ya Real Madrid kwenye msimamo wa LaLiga.

El Bilal Toure alifunga bao pekee katika mchezo huo na kumaliza rekodi ya Barca ya kutopoteza michezo 13 mfululizo kwenye LaLiga na kuwapa vinara hao kichapo cha pili pekee cha ligi msimu huu.

Kupoteza huko kunawaacha Barca wakiongoza kwa pointi saba mbele ya Madrid, ambao walikuwa wametoka sare ya bao 1-1 na Atletico Madrid Jumamosi.

"Nina hasira sana," alisema Xavi baada ya mechi.

"Ilikuwa mechi mbaya zaidi msimu huu kwa mtazamo wangu, zaidi ya yote katika kipindi cha kwanza.

"Ilikuwa ni siku ya kutoa tamko kwenye LaLiga na hakuna kisingizio. Hakukuwa na nguvu, hakukuwa na hata nia ya kushinda na hilo linanitia wasiwasi. Tuliteleza na tunawaomba radhi mashabiki. Kama tunataka kushinda LaLiga, lazima tubadilike.

"Kwa bahati nzuri tuna pointi saba, lakini tunajua itakuwa vigumu kushinda LaLiga. Kipindi cha kwanza ndicho kitu ambacho kimenikatisha tamaa sana msimu huu. Tulionyesha imani kipindi cha pili, lakini kipindi cha kwanza kilinikasirisha ."

Kipigo hicho cha kushtukiza kinachukua wiki ya kusikitisha kwa Barcelona, ambao walitupwa nje ya Ligi ya Europa Alhamisi na Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Mambo si rahisi kwa Wakatalunya hao, ambao watasafiri kumenyana na Real Madrid katika mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Copa del Rey siku ya Alhamisi.

Bado watakuwa bila Pedri na Ousmane Dembele ambao wote walikosa mchezo wa Almeria na majeraha, lakini Ansu Fati anaweza kurejea.

"Bila shaka tutajiinua," Xavi alisema. "Watu hawawezi kufikiria tutashinda LaLiga kirahisi. Itakuwa ngumu sana kushinda mataji. Tunashindana na bingwa wa sasa wa LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya (Madrid).

"Sisi ni Barca, lakini tunapaswa kucheza kwa bidii zaidi na hatutakiwi kukata tamaa kwa sasa."

# De Gea: Man inaweza kushinda mataji zaidi


**MANCHESTER, England**

DAVID de Gea anaamini kuwa Manchester United inaweza kuongeza mataji zaidi baada ya kutwaa Kombe la EFL msimu huu kwa kuifunga Newcastle United kwenye fainali katika Uwanja wa Wembley, Jumapili.

Bao la kichwa la Casemiro na la kujifunga la Sven Botman liliwezesha vijana wa Erik ten Hag kuvunja ukame wa miaka sita kwa ushindi wa mabao 2-0.

De Gea, ambaye alivunja rekodi ya kipa mwenzake Peter Schmeichel ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao akifikisha 181, aliongeza medali nyingine kwenye mkusanyiko wake hapo United.

Lakini huku klabu hiyo ikiwa bado inapigania mafanikio katika Ligi Kuu England, Kombe la FA na Ligi ya Europa msimu huu, Mhispania huyo ana matumaini kwamba wanaweza kuendelea kushinda.



"Bado tuko kwenye mashindano matatu na tuna nafasi ya kushinda mataji zaidi," alisema akiiambia BBC Radio 5 Live. "Ninahisi mawazo ya timu ni ya kushinda.

"Nimekuwa hapa kwa muda mrefu, kwa hiyo ina maana kubwa kwangu. Nina hisia kwa sababu imepita muda mrefu bila kombe. Nina furaha hapa kwa mashabiki.

"Tumekuwa katika fainali kadhaa ambazo tulipoteza, kwa hiyo tulijua leo (juzi) tunapaswa kufanya hivyo. Tulikuwa dhidi ya upande mgumu, lakini ninajivunia timu."

Alipoipita rekodi ya Schmeichel, De Gea alikiri kuwa alifurahishwa na mafanikio hayo, ingawa alisisitiza kuwa ni juhudi za pamoja.

"Kushinda fainali na kuvunja rekodi siku hiyo hiyo ni jambo lisiloelezekana, naipenda timu hii, kwa hiyo ni wakati mzuri."

## HABARI MICHEZO

326,057/-

# SIMBA SASA YAIGEUKIA AFRICAN SPORTS FA CUP

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi katika mechi iliyopigwa Uwanja wa St Mary's Chitende, Entebbe nchini Uganda dhidi ya Vipers, Klabu ya Simba sasa imeigeukia African Sports itakayopambana nayo keshokutwa, Alhamisi.

Katika mechi hiyo ya Kombe la FA hatua ya 16-bora, Simba itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kusaka timu itakayotinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa wake anaiwakilisha nchi kwenye michuano la Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mgunda, alisema pamoja na kwamba wana mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers hapa nchini Jumanne ijayo, lakini wanaichukulia kwa umuhimu wa pekee mechi yao dhidi ya African Sports.

"Tuna mechi zingine mbili mbele, zote ngumu, kwa kuwa malengo yetu ni kufanya vizuri, tuna mechi ya marudiano na Vipers, lakini kabla ya hapo tutacheza Kombe la FA dhidi ya African Sports. Mechi ni mechi na haya ni mashindano, hatuidharau timu yoyote kwa sababu hata hao African Sports haikupigiwa kura hapo ilipofikia.

"Imefanya hivyo kwa uwezo wake, pia walishinda hadi wamefika hapo kwa hiyo ni mchezo kama mwingine, tutajianda kisawasawa kama tunavyocheza mechi zote za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa," Mgunda alisema.

"Unajua mechi hizi ni mtoano na mechi za aina hizo hazina mwenyewe, inategemea siku hiyo mfumo wa kocha umekubali na wachezaji wamefanikiwa kuupambania, na timu inayofungwa inatoka moja kwa moja, hakuna marudiano, kwa maana hiyo tunaichukuliwa kwa umuhimu wa kipekee," alisema Mgunda.

Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya 16-bora ya kombe hilo kwa kuichapa Coastal Union pia kutoka Tanga bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa bao la Sadio Kanoute. Kwa upande wa African Sports imeweza kufika hatua hiyo kwa kuiondosha New Dundee ya Dodoma kwa mikwaju ya penalti 4-2, mechi ikichezwa Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

**MBIO...**



Washiriki wa mbio za tiGO Half Marathon (kilomita 21), wakianza mbio hizo katika mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YAPANIA 6 KWA BAMAKO

INATOKA UK. 24

ufundi kazi yake kwa sasa ni kwenda kufanyia kazi kikosi chao kuimarisha zaidi kila idara kuwa fiti.

Mchezo ujao wa Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga itaikaribisha Real Bamako Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano ya wiki ijayo kabla ya Machi 19 kushuka tena dimbani hapo kuvaana na wababe wao, US Monastir ya Tunisia.

Yanga itamalizia ugenini mechi zake za hatua ya makundi kwa kucheza na TP Mazembe ambayo mchezo wa awali miamba hiyo ya DR Congo ilikubali kipigo cha mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kikosi cha Yanga kiliondoka jana nchini Mali kuelekea Ethiopia ambapo kitalala hapo kabla ya leo kuanza safari ya kurejea jijini Dar es Salaam.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/03/23 | 20:30 | Southampton FC vs Leicester City | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 04/03/23 | 20:30 | Tenerife CD vs SD Eibar | 2.36 | 2.80 | 3.40 |
| 03. 04/03/23 | 20:45 | FC Volendam vs FC Emmen | 2.60 | 3.35 | 2.60 |
| 04. 04/03/23 | 22:45 | ACF Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 05. 04/03/23 | 22:45 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 06. 04/03/23 | 23:00 | CD Mirandes vs Real Oviedo | 2.48 | 2.90 | 3.15 |
| 07. 05/03/23 | 14:30 | Spezia Calcio vs Hellas Verona | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 08. 05/03/23 | 15:30 | Hansa Rostock vs Karlsruher SC | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 09. 05/03/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Espanyol Barcelona | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/03/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Everton FC | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 11. 05/03/23 | 19:30 | Liverpool FC vs Manchester United | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 05/03/23 | 19:30 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 05/03/23 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 14. 05/03/23 | 21:00 | Santa Clara Azores vs Vitoria SC Guimaraes | 2.70 | 3.15 | 2.60 |
| 15. 05/03/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Go Ahead Eagles | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 16. 05/03/23 | 22:45 | AS Roma vs Juventus Turin | 2.37 | 3.05 | 3.10 |
| 17. 05/03/23 | 22:45 | Stade Rennes vs Olympique Marseille | 2.75 | 3.35 | 2.45 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 28/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5060 | Lernayin Artsakh vs Alashkert Martuni | 5.17 | 3.31 | 1.65 |
| 14:30 | 2481 | Nassaji Mazandaran vs Esteghlal Tehran | 4.25 | 3.01 | 1.88 |
| 14:45 | 2277 | Geylang Int. vs Young Lions | 1.23 | 6.14 | 7.57 |
| 15:00 | 1908 | KS Lechia Zielona Gora vs Legia Warszawa | 12.42 | 5.59 | 1.19 |
| 15:00 | 1936 | Jedinstvo BP vs Jezero | 1.63 | 3.52 | 4.97 |
| 15:45 | 2479 | Alshoulla vs AL Akhdood | 4.32 | 2.98 | 1.84 |
| 15:50 | 1275 | AL Riyadh vs Al Qadisiyah | 2.00 | 2.88 | 3.80 |
| 16:00 | 1139 | Komarno vs Spartak Trnava | 3.37 | 3.32 | 1.99 |
| 16:00 | 1303 | AL Arabi (SA) vs Ohud Medina | 1.80 | 3.14 | 4.22 |
| 16:00 | 3032 | Sutjeska vs Iskra | 1.44 | 3.89 | 6.65 |
| 16:00 | 4633 | Ethiopia Electricity vs Sidama Bunna SC | 2.70 | 3.06 | 2.48 |
| 16:00 | 4648 | Rudar Pljevlja vs Buducnost | 5.78 | 3.67 | 1.53 |
| 16:30 | 1699 | Mohammedan SC vs Rajasthan United | 1.58 | 3.64 | 4.93 |
| 16:30 | 3488 | Bsk Bijelo Brdo vs HNK Sibenik | 3.36 | 3.36 | 1.98 |
| 17:00 | 2735 | FK Arsenal Tivat vs Mornar Bar | 2.75 | 3.06 | 2.44 |
| 17:00 | 4091 | Hermanstadt vs Universitatea Cluj | 2.40 | 2.97 | 2.97 |
| 18:00 | 5132 | Radnicki Nis vs Vojvodina | 2.55 | 2.90 | 2.48 |
| 18:30 | 2869 | Denguele Sport vs Bouake FC | 2.36 | 2.70 | 3.27 |
| 19:00 | 1880 | Chindia Targoviste vs U Craiova SA | 2.62 | 2.99 | 2.67 |
| 19:00 | 2457 | Slaven Belupo vs Rudes Zagreb | 1.50 | 4.04 | 5.38 |
| 19:30 | 3233 | FC Krasnodar vs CSKA Moscow | 2.84 | 3.25 | 2.27 |
| 19:30 | 4853 | Pogon Siedlce vs Gornik Leczna | 3.10 | 3.36 | 2.08 |
| 20:30 | 3072 | Aarhus Fremad vs Nordsjalland | 5.81 | 4.67 | 1.40 |
| 20:30 | 5407 | Cremonese vs Roma | 4.89 | 3.47 | 1.67 |
| 21:30 | 1039 | Farul Constanta vs Sepsi Osk | 2.08 | 3.18 | 3.39 |
| 22:00 | 4459 | Utrecht vs SV Spakenburg | 1.16 | 6.23 | 12.47 |
| 22:15 | 1873 | Stoke City vs Brighton | 5.87 | 4.11 | 1.47 |
| 22:15 | 3642 | FC Thun vs BSC Young Boys | 5.34 | 4.21 | 1.46 |
| 22:30 | 2040 | Cosenza vs Reggina | 3.87 | 3.24 | 1.91 |
| 22:30 | 2253 | Parma vs Pisa | 2.17 | 3.15 | 3.20 |
| 22:30 | 2552 | Leicester vs Blackburn | 1.36 | 4.60 | 7.04 |
| 22:30 | 5684 | Palermo vs Ternana | 2.00 | 3.34 | 3.45 |
| 22:45 | 1040 | AFC Wimbledon vs Stevenage | 3.56 | 3.07 | 2.03 |
| 22:45 | 1091 | Eastleigh vs York City | 1.95 | 3.41 | 3.57 |
| 22:45 | 2043 | Portsmouth vs Bolton | 2.62 | 3.31 | 2.52 |
| 22:45 | 2106 | Mechelen vs Zulte Waregem | 2.06 | 3.36 | 3.31 |
| 22:45 | 2110 | Gillingham vs Bradford City | 2.72 | 3.05 | 2.47 |
| 22:45 | 2261 | Fulham vs Leeds | 2.07 | 3.37 | 3.17 |
| 22:45 | 2469 | Harrogate vs Northampton | 3.21 | 3.16 | 2.12 |
| 22:45 | 2518 | Lincoln vs MK Dons | 2.27 | 3.18 | 3.08 |
| 22:45 | 3452 | Wrexham vs Chesterfield | 1.64 | 3.94 | 4.52 |
| 22:45 | 3793 | Dundee FC vs Partick Thisle | 1.76 | 3.60 | 4.01 |
| 22:45 | 3797 | Juventus vs Torino | 1.68 | 3.49 | 4.81 |
| 22:45 | 4057 | Peterborough vs Charlton | 1.75 | 3.75 | 4.15 |
| 22:45 | 4567 | Tranmere vs Crawley Town | 1.66 | 3.60 | 4.58 |
| 22:45 | 4608 | Preston vs Coventry | 2.55 | 3.19 | 2.60 |
| 22:45 | 5111 | Glentoran Belfast vs Glenavon | 1.34 | 4.63 | 6.80 |
| 23:00 | 1544 | Bristol City vs Manchester City | 11.73 | 6.65 | 1.16 |
| 23:00 | 2194 | Luton Town vs Millwall | 2.20 | 3.15 | 3.15 |
| 23:10 | 2697 | Lyon vs Grenoble Foot | 1.28 | 5.36 | 9.33 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Februari 28, 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Salah sasa anukia kutimka Liverpool

ANAO ANAO...



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya, akikokota mpira dhidi ya beki wa Real Bamako, Moussa Coulibaly, wakati timu hizo zilipokutana kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa nchini Mali juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAPANIA 6 KWA BAMAKO, US MONASTIR

●●●Yasema hesabu zote sasa kukamilikia kwa Mkapa baada ya kushindwa kutoka na tatu Mali huku...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvuna pointi moja ugenini dhidi ya Real Bamako ya Mali, Yanga imesema kazi kubwa iliyopo mbele yao kwa sasa ni kuvuna alama sita nyumbani katika michezo miwili ijayo.

Yanga juzi iliambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya Real Bamako ugenini, hivyo kufikisha jumla ya pointi nne katika Kundi lake la D la Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa nafasi ya pili nyuma ya US Monastir yenye pointi saba.

Akizungumzia mchezo huo na ijayo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia Nipashe kuwa wachezaji walipambana katika mchezo dhidi ya Real Bamako na sasa wanajipanga kwa ajili ya mechi mbili za nyumbani.

Kaze alisema mchezo ulikuwa mgumu na jinsi walivyopambana walikuwa na dhamira ya dhati kuondoka na pointi zote tatu, lakini haikuwa bahati yao baada ya wapinzani kusawazisha dakika za mwisho.

Alisema Real Bamako walicheza vizuri na wachezaji walionekana kucheza kiufundi zaidi na kufanikiwa kutumia upungufu wao kusawazisha.

"Mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa, wachezaji walipambana kutafuta pointi tatu ila haikuwa bahati, sasa tumebakiza mechi tatu, mbili za nyumbani tunahitaji kushinda hizo ili kupata nafasi ya kucheza hatua ya robo fainali.

"Ninaimani na wachezaji wangu tunaweza kufanya vizuri na kufikia malengo ya kucheza robo fainali endapo tukipambana na kupata matokeo mazuri ya ushindi mechi za nyumbani," alisema Kaze.

Aidha, aliwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi katika michezo hiyo ya nyumbani ili kutumia vizuri nafasi zao kama mchezaji wa 12 na kwamba benchi la

INAENDELEA UK. 23

## Kakolanya akaribia kung'olewa Simba

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaendelea kuiboresha safu yao ya ulinzi, uongozi wa Singida Big Stars upo mstari wa mbele katika mbio za kuinasa saini ya kipa namba mbili wa Simba, Beno Kakolanya, imefahamika.

Singida Big Stars tayari wameanza mchakato huo baada ya msimu huu kupata wakati mgumu katika eneo la kipa na tayari ikielezwa wameweka dau nono mezani kwa Kakolanya, ambaye mkataba wake umebaki miezi minne kufikia ukingoni.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jana kutoka kwa kigogo mmoja wa Singida Big Stars, zimeeleza kuwa Kakolanya amewekewa mezani mkataba wa miaka miwili na dau la Sh. milioni 100 kama ada ya usajili huku klabu hiyo ikiwa tayari kumlipa mshahara kiasi Sh. milioni tano kila mwezi.

Mtoa habari huyo alisema hatua hiyo ni baada ya wiki iliyopita Kakolanya kukutana na Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, kwa ajili ya mazungumzo ya kumwongezea mkataba huku ikidaiwa kuwa aliwekewa mezani Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaini mkataba na mshahara milioni sita kwa mwezi.

"Ni kweli Kakolanya mkataba wake uko ukingoni na Singida Big Stars wanahitaji huduma ya kipa huyo na wanahitaji kusaini mkataba wa awali wa miaka miwili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kwa msimu ujao.

"Hatua hiyo ya kuhitaji huduma ya kipa huyo wa Simba ni baada ya kuondoka kwa Metacha Mnata kwenda Yanga na Singida Big Stars kukosa mwingine wa uhakika, hivyo wanaimani na uwezo wa Kakolanya," alisema mtoa habari huyo huku akiomba hifadhi ya jina lake.

Gazeti hili lilimtafuta Kakolanya, ambaye alikiri mkataba wake kufikia ukingoni na kwamba ni kweli amepokea ofa ya timu mbili moja ya ndani na nyingine ya nje, kutoka Saudi Arabia.

Alisema kabla ya kufanya mazungumzo na klabu hizo, kwa sasa wanaendelea na mazungumzo na uongozi wa Simba ambao ni waajiri wake wa sasa na kwamba wameonyesha nia ya kuendelea kuhitaji huduma yake.

"Mkataba wangu na Simba umebaki miezi minne kufikia tamati na tupo kwenye mazungumzo na uongozi wangu ambao ninawapa kipaumbele kwa sasa kabla ya kwenda kuzungumza na klabu zingine," alisema Kakolanya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >